

KUTHIBITISHWA

KWA LILE AGIZO

 Mwaweza kuketi. Ni, nilikuwa nimejisahau kabisa, nikisikiliza ushuhuda, hata nikasahau kuushughulikia umati. Nina furaha sana kuwa hapa usiku wa leo katika ibada ya Bwana, kuweza kukutana na Ndugu O'Donnell. Na nilikuwa nikiangalia hili, wakiashiria hizo ishara kwa viziwi na bubu.

² Naye huyo ndugu alikuwa akiniambia, yule mama hivi majuzi usiku aliyekuwa kwenye kiti cha magurudumu, aliyekuwa na ile kansa kubwa juu yake, kwamba namna *hiyo*, ya kwamba aliponywa kimiujiza sana hata alikuwa ametoka kwenye kiti cha magurudumu, kansa imetoweka, naye ana wakati mzuri sana. Nami nilishukuru sana kwa jambo hilo.

³ Ni vema kuwa hapa usiku wa leo, Ndugu O'Donnell, na kwa kusanyiko hili zuri la watu. Hapa juu kwenye. . .

⁴ Hapa ni Tempe ama ni Mesa? [Ndugu mmoja anasema, "Tempe."—Mh.] Tempe. Tempe. Na sasa pote pamepanuka sana, kwa hiyo, karibu hapa, tangu nilipokuwa katika nchi hii, yapata miaka thelathini na mitano iliyopita, hata karibu sipajui mahali hapa tena.

⁵ Basi ni vema sana kuwa katika nyumba ya Bwana. Nilipokuwa nikiingia, m—msichana mdogo alisimama pale, ambaye ni maskini Binti O'Donnell, na—na maskini... wasichana wengine wawili wadogo, nao walikuwa wakizungumza nami mlangoni. Ndipo—ndipo nikasema, "Wananiambia kutaganda usiku wa leo hapa." Nikasema, "Ninyi wakusini karibu mgande hapa chini." Kwa hiyo msichana huyo mwingine akamwangalia huyo mwingine, kasema, vema, alikuwa ametoka Iowa, naye huyo mwingine akasema alikuwa ametoka Minnesota. Nami nikasema. . .

⁶ Kabla ya hapo, nilisema, "Nilipotoka nyumbani ilikuwa ni kumi na nne chini ya sufuri." Maskini msichana huyu kutoka Iowa, ama Minnesota, mojawapo, kasema, vema, ilikuwa hamsini na mbili chini wakati alipoondoka. Nikaja kugundua, nilikuwa mkusini. Hamsini na mbili chini. Tungalipata hiyo nchini mwangu, kwa kweli tungeganda. Hamsini na mbili chini, kwa namna fulani hiyo ni baridi, sivyo, inakuwa baridi hivyo?

⁷ Sasa, tunayahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu kuwa hapa pamoja nanyi, usiku wa leo, wakati huu wa ushirika kabla tu ya ule mkutano mkubwa wa Wafanyabiashara. Hiyo ni kusema, huo mkutano mkubwa utaanza Alhamisi hii ijayo, huko chini Ramada. Iko kwenye Mtaa wa Mashariki wa Van Buren.

Na bila shaka tunawaalikeneni nyote huko chini. Kutakuwako na wahubiri wa ajabu kwenye huo mkutano mkubwa. Naye Ndugu Velmer Gardner ni mmoja ninayemjua, halafu ninafikiri wana baadhi ya wafanyabiashara ambao watahubiri. Na ni—ninaamini Jim Brown alikuwa ni mmoja wao, na Dk. Reed, na, hakika, Ndugu Rose sikuzote yuko kule, Ndugu Osteen kutoka Texas.

⁸ Na kwa hiyo nina hakika mtakuwa na wakati mzuri sana katika kuja kule chini. Kweli tumesisimkwa, kwa kuungojea huu mkutano mkubwa. Natumaini utakuwa kama ulivyokuwa wakati ule mwingine, ila tu mkubwa zaidi. Basi kumbukeni, ni njoo mmoja, njoni nyote. Kila mtu amealikwa.

⁹ Na tena, yakiwa ni mapenzi ya Bwana, nafikiri nina wakati mdogo uliotengwa ambapo wataniruhusu nijaribu kuhubiri tena kwenye—kwenye kiamshakinywa Jumamosi asubuhi, nafikiri, nao ule mkutano Jumapili alasiri, hiyo ni kusema, Bwana akipenda. Na kwa hiyo nayahesabu hayo kuwa majaliwa makuu, kuweza kusimama pamoja na watu hao mashuhuri na—na kutoa ushuhuda kwa Bwana, kwa ajili ya Bwana, hasa.

¹⁰ Nami naomba ya kwamba Bwana atambariki Ndugu O'Donnell hapa, na kundi hili zuri la Wakristo hapa, wanaosafiri, wakimngojea Bwana. Kwa kuwa, kwa kweli, sisi ni wasafiri. Sisi ni wasafiri na wageni. Haya si makazi yetu. “Bali tunautafuta Mji ambao Mjenzi na Mbuni wake ni Mungu.” Nasi ni wasafiri tu. Sisi si. . . Haya siyo makazi yetu. Tunapitia tu huku. Nalo linatupa majaliwa makuu sana.

¹¹ Labda kama nikiweka hii *hivi*, ndugu. [Ndugu Branham anairekebisha maikrofoni—Mh.] Inatupatia majaliwa mazuri sana. Hiyo ni afadhali? Aa—ha.

¹² Ni majaliwa mazuri sana kuwa hapa, kuweka wakati huu wa ushirika pamoja nanyi Wakristo wa ajabu. Basi niliposikia ya kwamba nilikuwa nimepewa majaliwa ya watu hawa mbalimbali, kwamba makanisa yaliyokuwa, yalikuwa yakiniruhusu kuyahubiria, kabla tu ya ule mkutano mkubwa, niliwazia, “Ni wakati mzuri sana kuonyesha shukrani zetu kwa vile madhehebu haya mbalimbali yameshirikiana katika nyakati zilizopita, katika huduma zangu kote ulimwenguni; Assemblies of God, Foursquare, Jesus Name, Church of God, na mengi, na walio huru kote ulimwenguni, wote wakija kama moja, na kwa utukufu wa Mungu.” Naye Mungu amekuwa akifanya mambo makuu miongoni mwao, nasi tunashukuru. Halafu kurudi ambapo tunaweza kuyaelezea mawazo ye—yetu na ushirika wetu.

¹³ Na kama nilivyokuwa nikinukuu jana usiku, huku kwenye Maskani ya Ushirika ambako tulikuwa na ibada; basi nilikuwa na rafiki wa kale, Ndugu Bosworth. Wengi wenu mnamkumbuka

Ndugu Bosworth. Naye alikuwa akiniambia, akasema, “Ndugu Branham, unajua ushirika ni kitu gani?”

Nikasema, “Nafikiri najua, Ndugu Bosworth.”

¹⁴ Kasema, “Ni jamaa wawili katika meli moja.” Kwa hiyo, naam, yeye alikuwa mcheshi. Nami daima nilipenda hilo, “Jamaa wawili katika meli moja.” Kwa hiyo, sikuzote, blanketi huenea kidogo kumsaidia jamaa huyo mwingine, mwajua, na hilo ni zuri sana.

¹⁵ Sasa, hakika ninatumaini ya kwamba mtaniombea. Nami, leo hii, nilimtumia mwanangu huku juu muda kidogo uliopita aone kama kulikuwako na mtu yeyote aliyetaka kuombewa. Kwa kweli sikuja kufanya ibada za uponyaji, ni kuninii tu, loo, kuhubiri. Mtu yeyote anajua mimi si mhubiri, aliyewahi kunisikia. Lakini sina elimu, na siwezi kuhubiri. Lakini mimi—mimi kwa kawaida huwaombea wagonjwa. Ba—basi nikija, kwa kawaida watu hukusanyika wapate kuombewa. Hakika, kuna watu wengi sana walio wagonjwa. Bali Jumapili sikutaja kitu kulihusu, kwa sababu ningewaita watu kutoka makanisa mengine, kuja kwenye makanisa fulani haya niliyokuwa nikiyaendea Jumapili, wakaombewe, nami nikafikiri huenda likayadhuru baadhi ya makanisa hayo mengine, kwa hiyo nikaachana tu nalo.

¹⁶ Sasa, jana usiku nilitangaza ya kwamba usiku wa leo tungewaombea wagonjwa hapa juu. Basi Mungu akipenda, huenda ikawa kesho usiku ama usiku unaofuata, mojawapo, tutawaombea wagonjwa tena. Kwa hiyo natumaini ya kwamba itakuwa ni sawa, kwamba Bwana atamponya kila mtu aliye mgonjwa hapa usiku wa leo.

¹⁷ Nami nakwambia, rafiki yangu wa thamani, juu ya mambo yote ninatumaini ya kwamba wenye ugonjwa wa dhambi wataponywa usiku wa leo. Mnaona? Bwana akiwaponya maradhi yenu, nyinyi labda, mkiishi wakati wowote, mtakuwa wagonjwa tena. Mnaona? Lakini Uzima wa Milele ndio tunaoutafuta, hiyo ni kweli, kwa kuwa huo—huo ndio tiba halisi. Nami natumaini kama kuna mtu hapa ambaye si mwaminio katika Kristo, atakuwa mwaminio usiku wa leo.

¹⁸ Na kama uko hapa na hujazaliwa mara ya pili, ama kumpokea Roho Mtakatifu, hujajazwa na Roho Mtakatifu, ninatumaini ya kwamba huu utakuwa ndio usiku ambao hilo litatukia.

¹⁹ Endapo umerudi nyuma, natumaini ya kwamba Bwana Yesu atafanya jambo fulani halisi sana usiku wa leo, kwako hapa, na kuutia joto—kuutia joto moyo wako hivi kwamba, utarudi tu kwenye ushirika Wake tena, maana Yeye anangoja, kwa mikono iliyonyoshwa, kungojea.

²⁰ Nilihubiri miaka kadhaa iliyopita juu ya somo dogo wakati mmoja, huko katika Hekalu la Angelus, wakati

walipokuwa na yubile ya kipentekoste, miaka hamsini ya yubile. Ninakumbuka usiku wa kwanza, ambapo nilihubiri juu ya utakatifu, ambao ninauamini. Na kidogo sikutarajia hilo, bali, mwajua, kuwakatakata watu tu, na jinsi ambavyo watu walikuwa wameiondokea ile pentekoste asili. Kama wakati, hapo mwanzo, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka, jinsi watu hao walivyoyaishi yale maisha, yale waliyofanya, miaka hamsini iliyopita!

²¹ Nikasema, “Loo, tumetoka mbali. Tunayo madhehebu makubwa tangu hapo, mijengo mikubwa ya kupendeza, na wahubiri wakuu walioadibishwa.” Nikasema, “Nashangaa kama tungali tunayo baraka ya kipentekoste tuliyokuwa nayo wakati huo?” Mnaona? Mnaona? Nikasema, “Ilikuwa kwamba, dada ze—zetu walipokuja kanisani, ilikuwa ni aibu kwa mmoja wao kuwa na nywele fupi, amejipaka rangi makucha, ama kitu kama hicho. Lakini, hilo, walilegeza mambo mahali fulani.”

²² Na kwa hiyo kulikuwako na rafiki yangu, ambaye, yeye ni ndugu mpentekoste pia, na wengi wenu huenda mnamfahamu. Jina lake ni William Booth-Clibborn. Vema, wengi wenu mnamfahamu.

²³ Naye Ndugu Booth ni rafiki msiri wangu, ila tu hatukubaliani juu ya mafundisho, kwa sababu yeye ni mwenye—mwenye mawazo ya Kikalvini sana hata ana mawazo yanayonizidia mimi. Kwa hiyo ninaweza tu kuwazia Kikalvini mradi tu kitakaa kwenye Biblia. Mnaona? Halafu wakati kinapotoka humo, kimepita mawazo yangu; siwezi kuwaza tena.

²⁴ Kwa hiyo nilimwona jukwaani. Basi hapo tulipoondoka jukwaani, yeye alikutana nami huko nje, ndipo akaniangalia. Akasema, “Tsk, ts, ts, ts, ts. Aibu kwako. Ujumbe wa kisheria jinsi hii. Ulijua vema kuliko hivyo.” Alinirarua tu kabisa, mwajua.

²⁵ Kisha kesho yake nikahubiri juu ya *Mwana-Kondoo Na Hua*. Na kwa hiyo Bwana kweli aliubarikia maskini ujumbe huo mdogo, uliovonjikavunjika. Ndipo nilipotoka nje, yeye alikuwa akiyapangusa macho yake, mwajua. Akasema, “Ulikuwa ni mzuri, bali rahisi sana.” Rahisi sana! Nikasema. . . “Ulikuwa ni sawa,” kasema, “bali rahisi sana.” Yeye alikuwa ninii sana. . . Anaweza kuhubiri katika lugha saba, mwajua, kwa hiyo maskini mazungumzo yangu ya Kentaki yalikuwa ni rahisi sana kwake. Si ajabu, Desturi Nzuri Sana zisingemgusa popote, mnaona.

²⁶ Kwa hiyo hivyo karibu ndivyo inavyonibidi kuzungumza: kirahisi. Ninaamini Injili ni rahisi. Biblia ilisema, “Ni rahisi sana hata mpumbavu hapaswi kukosea.” Mnaona? Kwa hiyo ki—kile tu unachopaswa kufanya ni kukumbuka ABC. Mnajua kile hizo zinamaanisha? Daima Mwamini Kristo. [Kiingereza: Always Believe Christ.—Mf.] Hivyo tu ndivyo unavyopaswa kufanya.

Hilo latosha. ABC, nawe umeelimika kikamilifu, kadiri nijuavyo mimi.

²⁷ Kwa hiyo, sasa, kunao watu wanaosimama, nami ninalithamini hilo. Na sasa kamwe sikuja ku—kuhubiri. Nitawaombea wagonjwa. Lakini, kupata msingi kidogo, kuzungumza juu ya Maandiko.

²⁸ Nafikiri kidogo nilihubiri kupita kiasi, hivi majuzi asubuhi, kwa Ndugu Fuller. Nilipigia simu Maskani ya Uzima, ama kitu fulani. [Ndugu fulani anasema, “Maskani ya Imani.”—Mh.] Maskani ya Imani, nafikiri niliwachelewesha hivi majuzi usiku. Kabla sijafika kanisani, mchungaji ama mtu fulani alikuwa amenitumia habari, kasema, “Aisee, watu hawa wanapenda kwenda kulala usiku.” Kwa hiyo ni nadra sana mimi kuhubiri kwa zaidi ya saa sita ama nane, kwa hiyo kamwe sipiti hizo. Kwa hiyo, huko kwa Ndugu Outlaw, hivi majuzi usiku, nilifikiri karibu itamlazimu kunivuta aniondoe mimbarani. Kwa hiyo afadhali nisitumie nguvu nyingi sana usiku wa leo, huku juu kabisa, na baadhi yenu mkiwa mmetoka mbali sana.

²⁹ Sasa, ni vema kuwa hapa. Na kabla hatujalikaribia Neno sasa, hebu tuzungumze na Mwandishi wake.

³⁰ Mtu fulani alisema, sio muda mrefu uliopita, nilikuwa kwenye Maskani ya Injili ya Fort Wayne, B. E. Rediger. Alikuwa ni mtu mashuhuri wa Mungu, aliyekufa miaka kadhaa iliyopita, ambapo Bwana kweli alimbariki ndugu huyo. Alikuwa ni mtu hodari wa imani. Nilikuwa mvulana mdogo, nilikuwa nikiketi na Paul Rader kule, mhudumu mchanga tu.

³¹ Ndipo basi binti wa Ndugu Rediger akaingia wazimu, akawa kichaa. Siku moja alikuwa amerudi kwenye kibanda changu cha makaa kule chini, kwenye asubuhi moja ya Pasaka. Nao wakaniambia, “Msichana fulani mwendawazimu, kule nyuma kanisani.” Nami ndio kwanza nitoke kwenye uamsho mmoja. Nikarudi huko, nikakuta ilikuwa ni binti wa B. E. Rediger, naye Dada Rediger, ameketi pale. Nusura moyo wangu uzimie.

³² Basi alikuwa amesimama pale, akizichana nywele zake nzuri ndefu kwa vidole vyake, akipiga mayowe, “Nikeli ni nikeli. Peni ni peni.” Msichana mrembo. Wakati . . .

³³ Nikapiga magoti pale chini, na kusema, “Bwana Yesu, umrehemu.” Hilo lilitosha. Ameolewa na yuna watoto wawili ama watatu sasa, mzima tu. Mnaona? Basi ni neema jinsi gani, na rahisi.

³⁴ Sisi—sisi huangalia huko mbali sana hata tunafikia juu Yake, hakika, tukijaribu kupata kitu kilicho karibu sana nasi jinsi hiyo. Sisi, rahisi tu; tuamini; tuwe na imani; tusitilie shaka.

³⁵ Nilikuwa nikifanya mkutano kule. Ninamsahau huyo ndugu wa Kipentekoste aliye na mamlaka juu ya hiyo maskani sasa. Nami nilikuwa na mkutano kule. Na kulikuwako na wimbo

huu, *Amini Tu*, ulioandikwa na Paul Rader. Naye alikuwa ni Mkristo mzuri sana na mjumbe mkuu wa siku zake. Nilikuwa nimeketi kwenye chumba kidogo cha kusomea. Nao walikuwa wakiimba, nipate kuja jukwaani, kwa huo; ambao wameuimba, kote ulimwenguni. Na mimi—mimi nilikuwa nimeketi pale, na nikijua ya kwamba mumo humo katika chumba hicho cha kusomea ndipo Paul alipopata uvuvio wa kuandika wimbo huo. Nao huu hapa unaingia, *Amini Tu*. Loo, huo uliuchoma tu moyo wangu!

³⁶ Baada ya ibada kumalizika, kulikuwako na mambo mengi makuu Bwana wetu Yesu aliyokuwa amefanya mkutanoni. Nilirudi huko, karibu na mahali hapo, nami nilikuwa nikingoja.

Basi kulikuwako na mtu aliyeingia. Akasema, “Bw. Branham?”

Nami nikasema, “Naam, bwana.”

³⁷ Akasema, “Napenda kukusikia ukihubiri, bali,” kasema, “sarufi yako ni mbaya sana.”

Nikasema, “Naam, bwana. Najua hilo.”

Akasema, “Unasema baadhi ya mambo mabaya sana.”

³⁸ Nikasema, “Naam, bwana. Hiyo ni kweli.” Nikasema, “Sikupata nafasi ya kupata elimu.” Nikasema, “Nililewa katika familia ya watu kumi. Wazazi maskini, nami ilinibidi kwenda kazini mapema, kusaidia kuitunza familia hii. Hata sikupata elimu ya sekondari.”

Akasema, “Hicho si kisingizio sasa. Wewe ni mtu mzima.”

³⁹ Nikasema, “Vema, ninashughulika sana na kazi ya Bwana sasa, sina nafasi.”

⁴⁰ Kasema, “Hata hivyo, ungeweza kuchukua masomo kwa njia ya posta.” Kasema, “Sasa, kwa mfano, usiku wa leo, huko nje, wewe ulisema, ‘Ninyi watu wote mnaopitia kwenye mimbara hii.’”

⁴¹ Nikasema, “Kwani?” Sikujua tofauti yoyote. Nikasema, “Kwani hivyo sivyo alivyo?”

⁴² “La hashu.” Kasema, “Ilikupasa kusema ‘mimbara.’” Nikasema... Akasema, “Wewe...”

⁴³ Nikasema, “Vema, sawa.” Ni kitu fulani nilichokuwa nimekitamka vibaya, ama kitu fulani.

Akasema, “Vema, ni kwamba tu wewe huijui Biblia yako.”

⁴⁴ Nikasema, “Vema, huenda hiyo—hiyo ikawa ni kweli, bali ninamjua Mwandishi wake vizuri sana.” Nikasema, “Jambo ndilo hilo.”

⁴⁵ Mwajua, halisemi, “Kukijua Kitabu Chake.” Bali, “Kumjua Yeye ni Uzima.” Mnaona? Shetani analijua Neno Lake. Lakini, “Kumjua Yeye, Mwandishi wa Neno,” mnaona.

⁴⁶ Na tuviinamishe vichwa vyetu tunapozungumza na Yeye katika njia yetu nyenyekevu. Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, mioyo yetu, pamoja navyo, hivi kunayo haja maalum ambayo ungetaka tukukumbuke kwayo? Inua mkono wako kwa Mungu. Kwa moyo wako tu ishikilie haja yako, ukisema, “Bwana, ninahitaji wokovu. Ninahiaji uponyaji. Ni—ninahitaji jambo fulani.” Mungu ataelewa.

⁴⁷ Baba yetu wa Mbinguni, tunapoukaribia Uwepo Wako mtakatifu usiku wa leo, katika Jina la Bwana Yesu, tunakuja katika Jina Lake kwa sababu Yeye alisema, ya kwamba, “Ukimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalitenda.” Sasa, tunajua ya kwamba hatuwezi kuja katika jina letu wenyewe. Hatuwezi kuja katika jina la kanisa letu, katika jina la mchungaji wetu, wala katika jina la shirika letu, na kutarajia kusikiwa. Lakini tuna hakikisho kwamba kama tukija katika Jina la Bwana Yesu, ya kwamba Yeye alituahidi ya kwamba tungsikiwa.

⁴⁸ Nami naomba, usiku wa leo, Baba wa Mbinguni, ya kwamba kama vile tumekusanyika hapa katika maskani hii ndogo ambayo imewekwa wakfu kwa ajili ya utumishi Wako, ambayo mtumishi Wako, Ndugu yetu O'Donnell, anaichunga wakati huu, akiwachunga kondoo wanaokaa kwa muda katika sehemu hii ya nchi, ninaomba baraka Zako juu ya mchungaji huyu na juu ya familia yake, juu ya kanisa na kondoo wote wanaolishwa hapa malishoni.

⁴⁹ Ninaliombea kila kanisa lililowakilishwa hapa, kwa ajili ya watu wote. Na kwa ajili ya wale wasio Wakristo ninaomba ya kwamba usiku wa leo watakuwa Wakristo. Ninawaombea wafanyabiashara walio hapa, Ndugu Rose, Ndugu Williams, na wengine wengi, kwa ajili ya mkutano mkubwa ujao kule chini. Kwamba, uamsho huu mdogo wa siku hizi chache kote Phoenix, na Tempe, na Sunnyslopes, na kote nchini humu, utasababisha Wakristo wengi kushika upya, wengi waliorudi nyuma wakimrudia Mungu, wenye dhambi wengi wakimjia Kristo, wogonjwa wengi waponywe. Lijalie, Baba.

⁵⁰ Nena kupitia kwetu, kupitia kwa Neno usiku wa leo, ile Kweli. “Neno Lako ni Kweli.” Waponye wagonjwa wote na wanaoteseka, kimwili na kiroho pia. Mikono hii iliyoynuliwa ina haja, Bwana, nami naomba Wewe utakidhi hizo zote usiku wa leo, kupitia Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

⁵¹ Sasa, wengi wenu hupenda kuyasoma Maandiko pamoja na wale wanaosoma. Ningependa kusoma mahali pawili usiku wa leo. Moja ya hapo panapatikana katika Marko, mlango wa 16, na tutaanzia kwenye kifungu cha 14. Na hapo pengine panapatikana katika Yohana Mtakatifu. Ama, nafikiri hapo ndipo nilipoandika. Hebu nione, kwanza. Naam. Yohana Mtakatifu 14:12 ndipo penye Andiko la pili. Na sasa katika

Marko Mtakatifu, mlango wa 11 na kuanzia kifungu cha 14. Na Yohana Mtakatifu 14:12. Sasa tunataka kusikiliza hilo somo kwa makini, kwa sababu Neno la Mungu ndilo tunalotaka kusikia. Kwanza, Marko 16.

Ndipo baada ya hayo akaonekana na wale kumi na mmoja walipokuwa wakila, akawakemea kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa kuwa hawakuwasadiki wale waliomwona alipofufuka katika wafu.

Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.

Aminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.

Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; Katika jina langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya;

Watahika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, . . . watapata afya.

Basi . . . Bwana baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.

Nao wale wakatoka, wakihubiri kote kote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo. Amina.

52 Yohana 14:12, Yesu akizungumza.

Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, kubwa kuliko hizo atafanya; kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.

53 Ni—ningetaka kuchukua somo, Bwana akipenda, juu ya *Kuthibitishwa Kwa Lile Agizo*, kama somo, na kuzungumza tu. Ninayo Maandiko machache na muhtasari ulioandikwa, ambao huenda ukatusaidia tunapoendelea. Sasa: *Kuthibitishwa Kwa Lile Agizo*.

54 Sasa, nafikiri kwamba kitu chochote kinapaswa kuthibitishwa. Kama ukijenga nyumba, itabidi ijengwe kulingana na vipimo kamili, la sivyo hawataithibitisha nyumba hiyo kujengwa; nawe itakubidi kuibomoa tena, ujenge upya.

55 Nami nafikiri, pia, kama ulikuwa ukishuka kwenda barabarani, na, ama huko nje kazini mwako, na mtu fulani angekuja kwako na kusema, “Mimi ni mkuu wa polisi Marekani. Sasa ninakukamata, katika jina la ofisi yangu.” Sasa, unayo haki ya kumwambia mtu huyo . . .

56 Kama ulimwangua, yeye amevaa nguo rasmi, na amebandikwa beji. Hilo bado halimfanyi mkuu wa polisi Marekani. Mbabaishaji yeyote angeweza kuivaa hiyo. Unaweza

kununua beji hapa, karibu, kwenye duka la mali rahisi. Uende kwenye seli yoyote ya mitumba na kujinunulia nguo rasmi, ama chochote kile. Hilo halimfanyi mkuu wa polisi Marekani.

⁵⁷ Kujitambulisha, hana budi kuwa na makaratasi yake yaliyotiwa muhuri, yanayothibitisha tamshi lake kwamba ni mkuu wa polisi Marekani. Ama, yeye si kitu mpaka atakapothibitishwa kuwa ndivyo alivyo. Yeye amelithibitisha agizo lake, naye anafanya hivyo kwa tamshi lililotiwa muhuri, tangazo, kuonyesha ya kwamba mtu huyu ameapishwa. Naye amekuwa... Agizo lake limetiwa muhuri kwa muhuri wa Marekani, halafu juu ya jina lake. Nalo hilo linamfanya basi, kama amevaa beji, ama kama amevaa nguo rasmi. Mradi tu amebeba karatasi hii, yeye ni mkuu wa polisi, na hilo ndilo agizo lake. Beji tu na nguo rasmi hazitafanya kazi.

⁵⁸ Tunaona, mara nyingi sana, katika jeshi. Nimewasikia ndugu zangu na wengi wa hao waliokuwa katika nchi za ng'ambo. Kwamba, mara nyingi, Wajapani na Wajerumani, na hizo nchi zingine za kigeni ambazo zilikuwa adui zetu vitani, kama wanalitambua kuokota askari aliyekufa, basi wanachukua mmoja wa askari wao ambaye hiyo nguo rasmi ingemtosha, mbona, angeweza kumwiga askari wa Kimarekani. Naye ilibidi atambulishwe kikamilifu, la sivyo wasingeamini nguo yake rasmi ama labda kibandiko chake alichokuwa nacho shingoni mwake. Ilibidi atambulishwe kwamba alikuwa ni askari wa Kimarekani, kwa sababu kwa urahisi angeweza kuwa ni mpelelezi. Mpelelezi yeyote hafifu angeweza kuvaa nguo rasmi ya Marekani.

⁵⁹ Nasi tunaona hilo katika mienendo yote ya maisha. Tunaona hilo, leo hii, labda mtaani. Tunawasikia watu wengi wakisema ya kwamba wao ni Wamarekani.

⁶⁰ Na hapa wakati fulani uliopita, nikitoka kwenye Kwotamasta aliyekuwako kule Jeffersonville, nilikuwa nikitembea asubuhi moja, nikienda kufanya doria. Basi kulikuwako na ja-jamaa aliyevalia vizuri akitembea mtaani, sigara kubwa mno kinywani mwake, mfanyakazi wa serikali. Naye akaniangalia, asubuhi na mapema, huku amevaa miwani ya jua. Nikasema, "Habari za asubuhi, bwana."

Akanitazama, akasema, "Huh!" Akaanza kwenda zake.

⁶¹ Sasa, nikajiwazia. Sipaswi kusema chochote. Lakini, moyoni mwangu, yeye hakuwa Mmarekani halisi, maana kanuni za Marekani hazijawekwa msingi juu ya upuuzi kama huo. Kweli. Ushirika, na kuvumiliana, urafiki.

⁶² Na sasa, mnaona, wote wanaoishi Marekani sio Wamarekani. Kunao wapelelezi, wakomunisti, na kila kitu kingine. Na jinsi tu wanavyoweza kujulikana vizuri, kama wao ni wa kweli ama si wa kweli, ni kwa kile hasa, kile kilicho ndani yao, kama moyo wao uko Marekani ama kijidaftari chao tu cha mfukoni. Mnaona?

⁶³ Inategemea ni kitu gani. Mbabaishaji yeyote anaweza— anaweza kuwa na hati hizi za utambulisho, na bado asiwe ni mkweli.

⁶⁴ Hiyo ndiyo sababu ninaamini ya kwamba wote wanaokuja kwetu, wakijiita Wakristo, mabalozi waliotumwa kutoka Mbinguni, wanapaswa kuwa na thibitisho la agizo lao. Ninaamini kunapaswa kuwe na thibitisho la agizo lao.

⁶⁵ Sasa, tunatambua ya kwamba Yesu alisema hapa, katika Marko mlango wa 16, ya kwamba wote Yeye aliowatuma kwa agizo watakuwa na thibitisho. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

⁶⁶ Sasa, Yeye hakusema, “Hizo, labda zitafuata, ama huenda zikafuata.”

⁶⁷ Alisema, “Enendeni ulimwenguni mwote.” Sasa, mtu fulani anataka kulikata agizo hilo, miaka elfu mbili iliyopita. Lakini Yeye alisema, “Ulimwenguni mwote, kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuata ulimwenguni kote, na kwa kila kiumbe.” Mnaona? Na hizo zilikuwa ni ishara zitakazofuata, kuthibitisha huo utambulisho.

⁶⁸ Biblia ilisema, “Injili ilikuja kwetu sio kwa neno pekee, bali kwa nguvu, madhihirisho ya Roho Mtakatifu.” Kwa maneno mengine, “Ni Roho Mtakatifu akilichukua Neno la Mungu na kulidhihirisha.” Mnaona? Na, vinginevyo, njia pekee ambayo ishara za Marko 16 zingeweza kufuata mwaminio ni kwamba Roho Mtakatifu Mwenyewe alichukue Neno la Mungu na kulidhihirisha kwa watu. Jambo ndilo hilo. Sasa, imani hulifanya Neno hilo liishi. Mnaona?

⁶⁹ Neno ni Mungu. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.” Ndipo Yesu akasema, “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo, mtatendewa.” Mnaona? Hiyo ni kukaa pamoja na Kristo katika Neno. Usiende kulia wala kushoto. Dumu moja kwa moja pamoja nalo. Mnaona? Ndipo basi silo Neno lako hasa, basi. Ni Neno Lake, nalo Neno Lake lina nguvu na mamlaka nyuma Yake. Sasa, basi kama Roho Mtakatifu, ambaye ni Neno la Mungu, ama nguvu za Neno la Mungu, akiingia pamoja na Neno la Mungu, italifanya Neno la Mungu lijionyeshe Lenyewe.

... Enendeni ulimwenguni mwote, na mkadhihirishe Injili kwa kila kiumbe.

Na kila aaminiye na kubatizwa ataokoka;... asiyeamini atahukumwa.

Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio;...

⁷⁰ Ni picha nzuri jinsi gani hiyo! Kama tungeweza tu kuingia kwenye kilindi sasa na kusikiliza: huo ulikuwa ndio utambulisho uliokuwa uning’inie juu ya kila mtu aliyetoka kwenda kuihubiri

Injili. Wala hakuna mtu aliye na haki ya kuihubiri Injili pasipo na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Yesu asingemruhusu Petro, Yakobo, Yohana, yeyote wa hao wengine, kuihubiri Injili mpaka walipongojea katika mji wa Yerusalemu mpaka Roho Mtakatifu akawajaza, kwa sababu Roho Mtakatifu ndiye anayelifanya Neno la Mungu kuingia katika matendo. Mnaona?

⁷¹ Sasa, Neno lilo hilo li hai tu usiku wa leo kadiri lilivyokuwa ile saa liliyonenwa. Mnaona? Ninii... Yote tunayohitaji ni Roho Mtakatifu nyuma ya Neno, kulifanya Hilo litende kazi na kudhihirisha zile nguvu lilizoahidi. Kila baraka ambayo Mungu aliahidi, kila kitu alichosema Yeye, kinaweza kufanywa hai kama Roho Mtakatifu akiwa nyuma ya hilo Neno, kwa sababu hicho ndicho kitu kinacholihuisha Neno na kulipa uhai. Mnaona? Na sasa tunajua kwamba hilo ni kweli.

⁷² Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na wote ninaowatuma.” Wengine, hukataa. Hivyo tu. Hakika.

⁷³ Asiyeamini yeyote, mkosoaji yeyote wa Neno, anaweza kuja na utambulisho wa dhehebu fulani, dhehebu fulani la kubuniwa na mwanadamu ama kitu fulani, aseme, “Mimi ni Mpresbiteri, Mlutheri, Mbaptisti,” chochote kile. Yeye kwa urahisi angejitambulisha mwenyewe katika ushirika wa kanisa lilo hilo la kimadhehebu, kwa sababu ya hati zake za utambulisho. Lakini hati za utambulisho wake hutoka tu kwa dhehebu ambalo limefanyizwa kwa nadharia wala sio Neno la Mungu.

⁷⁴ Lakini Mungu, kama yeye ametumwa kutoka kwa Mungu, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Mnaona? Yesu alisema hivyo. Mnaona? Mnaona?

⁷⁵ Ni, ama, kama utachukua yale dhehebu fulani liliyosema, nadharia ya kubuniwa na mwanadamu iliyosema. Watahubiri fundisho la nadharia hiyo, halafu hizo ndizo hati zao za utambulisho kwa halmasharuri ya mashemasi, ama chochote kile, kwamba wana ushirika mzuri na dhehebu hilo. Sina neno dhidi ya hilo, mnaelewa.

⁷⁶ Ila ninatetea tu yale Yesu aliyosema. Mnaona? Yeye alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Naye Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 14:12, “Amin, amin, nawaambia.” Hiyo ni “Hakika, hakika, nawaambia, yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.”

⁷⁷ Basi mtu anawezaje kuamini ya kwamba ametumwa kutoka kwa Mungu, kisha ageuke na kulikana agizo lenyewe ambalo Mungu alisema lingekuwa, kwamba lingekuwa ndilo utambulisho wa kila mtu ambaye Yeye alimtuma? Mtu anawezaje kusema, “Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu”? Mtu anawezaje kusema, “Hakuna kitu kama kuwaponya wagonjwa”? Mtu anawezaje kusema, “Hakuna kitu kama kunena kwa lugha, kuwatoa pepo”? Wakati, hizo zilikuwa

ndizo hati zenyewe za utambulisho ambao Yesu alimbandika kila mwaminio ambaye angeninii, Yeye alimtuma. Hayo ndiyo mamlaka.

⁷⁸ Sasa, huenda ukaenda shuleni na kupata Ph.D., na LL.D., na lolote zaidi unalotaka kufanya, na hilo ni sawa. Huo ndio utambulisho wako kwa dhehebu hilo. Na hizo ni sawa. Sina neno dhidi yazo; laiti ningalikuwa nazo.

⁷⁹ Lakini utambulisho ambao Yesu, wakati Yeye anapomtuma mtu, ni, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Mnaona? Huo ni utambulisho ya kwamba alitumwa na Mungu. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

⁸⁰ Sasa, kama nilivyosema, mbabaishaji yeyote anaweza kuokota nguo rasmi ama beji, bali hizo hasa si hati za utambulisho. Hati za utambulisho ndizo muhimu, si nguo rasmi wala beji. Na kuna watu wengi. . . Na ni vibaya sana kwamba inanibidi kusema hili, bali ni kweli. Hatuna budi kuwa waaminifu. Kuna wengi mno wa . . . watu wetu wa Kipentekoste, wanaovaa tu beji na nguo rasmi, mnaona, kwa kuwa wanaishi tofauti sana na vile hasa pentekoste inavyopaswa kuwa, mpaka ha—hakuna kitu kwake. Hivyo tu. Na hilo linaleta tu shutuma kwenye Huduma. Hiyo ni kweli. Inawafanya watu kuwa na shaka.

⁸¹ Lakini Yesu alitoa ainisho, ya kwamba ingekuwa ni sawa, kwa sababu, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Hilo ni jambo moja. Roho Mtakatifu aliangalia chini kupitia mtiririko wa wakati na kuona ya kwamba wanaume wangelipotosha Neno Lake na kusababisha *hili*, *lile*, na *linginelo*, kwa hiyo Yeye akalifanya dhahiri sana na la kweli hivi kwamba hakuna njia ya kulikwepa. Alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sasa, tunajua hilo kwamba ni kweli.

⁸² Asiyeamini anaweza kubeba hati hizi za utambulisho za kimadhehebu, bali hizo sizo zinazomfanya mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu. Wanatembea kuzunguka hapa pamoja na kila namna ya vitabu chini ya mikono yao, kote nchini, na *hili*, *hili* la Yehova, na *fulani-fulani*, na yote *haya*, na *mengineyo*, bali hilo halilifanyi kweli. La, bwana.

⁸³ Yesu alisema, “Muwajaribu kwa Neno.” Hiyo ni kweli. Neno, “Ishara hizi zitafuata.”

“Unaamini katika nguvu za Mungu?”

⁸⁴ “Loo, kanisa le—letu linafundisha kwamba. . .” “Kanisa letu,” hilo halina uhusiano wowote Nalo.

⁸⁵ Ni yale Neno la Mungu lisemayo. Mnaona? Naam. “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.” Neno lililo hai, lililonenwa na Mungu aliye hai, halina budi kuwa katika kiumbe kilicho hai. Basi anawezaje mwanamume ama mwanamke, anayedai kuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu,

kukana yale Mungu aliyosema katika Neno Lake? Kwa sababu, ni Roho Mtakatifu yeye yule aliyeliandika Neno, ndiye Roho Mtakatifu yule yule anayenena kupitia mtu huyo. Hiyo ni kweli. Haina budi kuwa hivyo. Yeye hawezi, hawezi kufanya hivyo. Naam, bwana.

⁸⁶ Sasa, lakini, hiyo, huenda mtu fulani akaja na kusema, “Ninayo kadi ya ushirika. Mimi ni mfuasi wa kanisa *hili* ama kanisa *lile*.” Hilo lingali halilifanyi sahihi. Huenda akawa na Ph.D., LL.D., na chochote zaidi kutoka kwenye shule fulani maarufu. Hilo ni sawa. Sina chochote dhidi ya hilo. Hilo bado huenda likawa ni sawa. Sina neno dhidi ya hilo. Lakini kama Mungu alimtuma... Na kama akilikana agizo hili *Hapa...* Iwapo ana *hilo* kuongeza *Hili*, vizuri sana. Lakini endapo ana *hilo* bila *Hili*, basi halifai kitu. Mnaona? Hiyo ni kweli.

⁸⁷ Ni sawa kama mtu akivaa nguo rasmi na beji pamoja na hati za utambulisho. Vema. Ila anaweza kuvaa nguo rasmi na beji pasipo na hati za utambulisho. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo ni thibitisho la agano, ambalo halina budi kusimama. Halina budi, bila shaka.

⁸⁸ Asiyeamini huyu ambaye huenda akapitia hapa na kusema, “Vema, siamini kwamba kuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. Shule zetu zimefundisha ya kwamba—ya kwamba hizo siku zimepita. Haitupasi kuwa na huo tena.” Basi kuna wengi sana wanaoamini hilo. Kunao wengi sana wanaoamini hilo kwa unyofu, watu wazuri, ni kwa sababu kwamba wanaisikiliza shule badala ya Neno la Mungu. Hiyo ni kweli kabisa.

⁸⁹ Hapa wakati fulani uliopita, mahali fulani, kulikuwako na mwa—mwa—mwanamke fulani. Alikuwa na mwana. Naye alikuwa na wito wa Mungu maishani mwake; alionekana kuwa nao. Basi maskini huyo mama alitaka kumtuma shuleni, kufanya yote awezayo ili aweze kumjenga. Ambalo, hilo ni jambo jema la kufanya. Ila alimtuma kwa shule isiyofaa. Alimtuma mahali ambapo walianza kufundisha kinyume na Neno la Mungu, naye akaendelea. Alifua nguo, apate kumpeleka shuleni, na kadhalika, ndipo muda mrefu ukapita. Basi, hatimaye, hakuja nyumbani kwa muda.

⁹⁰ Maskini mama huyo akawa mgonjwa. Akawa mahututi sana, sana. Naye akawa hali mbaya sana hata madaktari wakasema hataishi, kwamba hana budi kufa. Kwa hiyo akamwomba mmoja wa majirani wake amtumie mwanawe telegramu, aje nyumbani mara moja, kwa sababu walikuwa wakimtarajia kufa. Na kwa hiyo huyo jirani akaituma hiyo telegramu.

⁹¹ Na—na kwa hiyo huyo mvulana akajiandaa kuja. Ndipo baada ya kitambo kidogo, telegramu nyingine ikarudi na kusema, “Usijali. Amepona.”

⁹² Kwa hiyo basi, miezi kadhaa baadaye, huyo mvulana akaja nyumbani kumtembelea mama yake. Na—naye akamwambia, akimfurahia, na kumwambia alikuwa na Shahada yake ya Sanaa, na yote aliyokuwa amefanya, na jinsi alivyoendelea vizuri shuleni. Kisha akasema, “Jambo lingine, mama,” kasema, “Nimesahau kukuuliza.” Kasema, “Ulinitumia telegramu, yapata miezi sita iliyopita, nije nyumbani.” Kasema, “Nilifadhaika sana.” Kisha kasema, “Nilifadhaika sana kulihusu.” Halafu kasema, “Nikajiandaa kuja. Ndipo basi telegramu nyingine ikaja, kwamba ulikuwa sawa. Ulikuwa umepona. Nami nilifurahia sana hilo. Mama, ningetaka kukwambia, ama, mama, ningetaka uniambie kilichofanyika. Ni dawa ya namna gani daktari aliyokupa, na ulikuwa na daktari gani?” Kasema, “Ningetaka kwenda na—na kumpongeza kwa ajili ya kazi yake nzuri.”

⁹³ Akasema, “Sawa kabisa, mwanangu.” Kasema, “Dk. Yesu Ndiye aliyefanya hivyo.”

Akasema, “Mama?”

⁹⁴ Kasema, “Dk. Yesu.” Akasema, “Dk. *Fulani-wa-fulani*, tabibu wangu, alikuja hapa, nayo homa yangu ilikuwa juu sana, nilikuwa nimerukwa na akili.” Kisha kasema, “Wao walisema nilizidi kudhoofika sana, kisha nilikuwa naenda kufa.” Naye akasema, “Unajua mahali ile misheni ndogo ilipo huko pembeni, huko chini vichochoroni?”

“Naam.”

⁹⁵ Kasema, “Hao watu walikuwa na mkutano wa maombi huko chini usiku mmoja, nao wakasema Roho Mtakatifu aliwaambia waje huku na kuniombea.” Kisha kasema, “Mara waliponiombea, homa yote ikaniacha.” Ndipo akasema, “Loo, mwanangu!” Akasema, “Haleluya!” Akasema, “Nimepona.”

⁹⁶ “Loo,” akasema, “mama, mama, ujasiri wenyewe! Mbona, hupaswi kushirikiana na watu kama hao.” Akasema, “Mbona, hupaswi kuwakaribisha hao watu huku juu.”

Akasema, “Loo, kwa nini, mwanangu?” Kasema, “Vema, utukufu kwa Mungu!”

⁹⁷ Yeye akasema, “Mama, usiseme mambo hayo.” Kasema, “Mbona, mbona, unanishtusha!” Mnaona? Kasema, “Mbona, hupaswi kusema mambo hayo. Mbona,” kasema, “hao watu hawana elimu. Hawajui lolote kuhusu Biblia.”

⁹⁸ “Loo,” akasema, “samahani, mwanangu.” Kasema, “Walishuka moja kwa moja na kunisomea kutoka kwenye Biblia, ambapo ilisema, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.’” Kasema, “Ngoja. Nimelisoma mara nyingi. Nimelitia alama kwenye Biblia yangu. Nitakuonyesha.”

“Loo, ngoja kidogo, mama.” Kasema, “Hiyo ni Marko 16.”

“Naam, hapo ndipo ilipo, kipenzi,” kasema, “Marko 16.”

⁹⁹ Kasema, “Loo, mama,” kasema, “unaona, watu hao maskini, hawajui vizuri.” Kasema, “Tulijifunza shuleni ya kwamba Marko 16, kuanzia mlango wa 9 na kuendelea, haijavuviwa. Unaona? Kweli haijavuviwa. Ilongezewa tu.”

¹⁰⁰ Ndipo maskini mama huyo akasema, “Utukufu kwa Mungu! Haleluya!” Na yeye. . .

Huyo mvulana akasema, “Mama, unamaanisha nini?”

Akasema, “Nilikuwa nikiwazia tu.”

Kasema, “Kuwazia nini, mama?”

¹⁰¹ Akasema, “Kama Mungu angeweza kunifanyia hivyo kwa Neno lisilovuviwa, angeweza kufanya nini na lile ambalo kweli limevuviwa?” Kwa hiyo, hiyo ni kweli. Mnaona? Mnaona? Jambo ndilo hilo. Loo, jamani!

¹⁰² Kulikuwa na shida gani? Misheni hiyo ndogo huko pembeni ilikuwa na hati ya utambulisho, labda sio Ph.D. ama LL.D. Ama. . . Lakini walikuwa na hati za utambulisho wa Mungu, “Pamoja na ishara hizi zikiwafuata waaminio.” Yesu alisema tutafanya hivyo. Wao, walikuwa na thibitisho la Mungu. Walikuwa na agizo Lake, kwenda kuweka mikono juu ya wagonjwa, nao wakafanya jinsi tu Yeye alivyosema wafanye, ndipo (wao) Mungu akalithibitisha Neno kwa ishara zilizofuata. Ni thibitisho kwamba wametumwa na Mungu. Naam, bwana. Hiyo ni kweli. Vema.

¹⁰³ Sasa, hilo ni somo zuri. Kwa sababu, mvulana huyo alikuwa ameondoka kwenda kusoma, na kweli alikuwa na Ph.D. yake, bali hao walikuwa na thibitisho la Neno. Yeye alikuwa na thibitisho la shahada kutoka kwenye chuo fulani, bali wao walikuwa na thibitisho la Neno la Mungu kutoka Mbinguni, pamoja na Roho Mtakatifu kuunga mkono yale waliyokuwa wakizungumzia. Naam, bwana. Ndipo Mungu akampa ishara. Naam, bwana. Loo, jinsi ninavyomshukuru Mungu kwa ajili ya jambo hilo! Watu wa Mungu daima wanazo hizo.

¹⁰⁴ Sasa, bila shaka, itampasa asiyeamini kuwa na sehemu ndogo ya Neno la Mungu, apate kuligeuza Hilo, kulifanya liendane na kanuni ya imani, lipate kufanyika danganyifu zaidi. Sasa, mwajua, uongo ulio mkubwa kuliko wote uliowahi kusemwa una Ukweli mwingi ndani yake. Hiyo ni kweli. Kumbukeni. Kila. . . Uongo wa kwanza uliowahi kusemwa, ulikuwa na asilimia tisini na tano ya Ukweli, wakati Shetani alipomwambia Hawa, katika bustani ya Edeni, “Mambo haya yote Mungu amesema.” Yeye alikubali, “Hiyo ni kweli.” Alikubali, “Hiyo ni kweli, kila kitu alichosema Mungu. Lakini,” kasema, “hakika hamtakufa.” Hilo hapo.

¹⁰⁵ Mtu fulani angaliweza kusema, “Hao walikuwa maskanini, hapa juu kwenye usiku huu *fulani-fulani*.” Naam. “Watu wote

walikusanyika mle.” Naam. “Wakaimba nyimbo.” Naam. “Ndipo mhudumu akahubiri.” Naam. Hiyo ni kweli. “Kisha wajua nini? Walipitisha chupa kuzunguka, nao wote wakalewa.” Uongo. Mnaona?

¹⁰⁶ Roho alishuka tu, wote wakalewa. Mnaona? Ni tofauti tu jinsi hiyo, mnaona, hapo hawakupitishiana chupa. Lakini baraka ya kiroho ya Mungu ilishuka juu ya hao watu. Wakapepesuka. Wakaanguka. Nao kweli walikatakata namna hiyo. Lakini chupa siyo iliyosababisha hilo. Ilikuwa ni Roho Mtakatifu akilithibitisha Neno Lake kwa ishara zilizofuata. Mnaona? Mnaona? Yote yalionekana ni kweli tu, ila ile chupa. Mnaona?

¹⁰⁷ Sasa, ningesema, ulikuwa kule? “Naam.” Hao watu walikuwako? “Naam.” Walipepesuka? “Naam. Naam.” Yote haya? “Naam.” Hayo yote ni kweli ila jambo hilo moja.

¹⁰⁸ Kwa hiyo hivyo ndivyo ambavyo asiyeamini, asiye-... mtu asiyetambulishwa na Mungu, yeye atasema, “Loo, ninaamini Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Ninaamini Mungu ndiye Baba wa Yesu Kristo. Ninaamini mambo haya mengine yote.” Mnaona? Bali inapofikia kwenye sehemu *Hii* nyingine, “Loo, *Hiyo* ni kwa ajili ya siku nyingine,” Mnaona? Huo hapo uongo wake. Hiyo ni kweli. Yeye anajaribu kugeuza sehemu ndogo ya Neno la kweli, kulifanya liwe danganyifu kwa watu.

¹⁰⁹ Lakini kitu gani? Yesu alifanya jambo hilo dhahiri. Yeye alisema, “Ishara hizi zitathibitisha Ujumbe ambao nimetuma.” Naam, bwana.

¹¹⁰ Nilikuwa mhubiri wa Kibaptisti wakati mmoja, ningali ninawapenda Wabaptisti. Lakini nilipata kitu hiki kingine. Mnaona? Sasa, silo—silo hasa. Ka—kanisa la Kipentekoste, sisemi ni kamilifu tu, hakuna kitu ndani yake. Bali ndilo zuri kuliko yote tulilo nalo, kwa hiyo hebu tudumu moja kwa moja nalo. Hivyo tu. Wao kweli wanaamini. Huenda baadhi yao wasiwe na imani ya kutosha.

¹¹¹ Mimi niko pamoja nao, bila imani ya kutosha kuyafanya Maneno yote yatinie. Bali kamwe sitamzuia mtu aliye na imani ya kutosha kutifanya zitimie. Kamwe sitajificha nyuma ya kutokuamini, katika kusema haliwezi kutendeka. Iwapo huyo mtu anaweza kulichukua Neno la Mungu na kulithibitisha kwa nguvu za Mungu, nasema, “Utukufu kwa Mungu! Bwana, niinue na uache nisimame, kwa imani, juu ya uwanda wa Mbinguni.” Naam. Hakika nitadumu na hilo.

¹¹² Wanafanya tu kidogo, kutosheleza kanuni yao ya imani. Lakini mtumishi wa Mungu anayo ishara Yake, kweli kabisa.

¹¹³ Agano la Kale, kulikuwako na mtu, wakati baadhi yao wasingeweza kuandika jina lao, kwa hiyo walikuwa na muhuri, nao ulikuwa ni ishara. Wangeitia muhuri, namna *hiyo*. Ikamalizika. Muhuri ni kazi iliyomalizika.

114 Waefeso 4:30 inasema, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwaye mmetiwa muhuri hata Siku ya Ukombozi wenu.” Ni kutiwa muhuri, kazi iliyomalizika; kwamba Mungu amekuona, akaitambua imani yako uliyokiri Kwake, akakumwagia Roho Mtakatifu, na kukutia muhuri hata Siku ya Ukombozi wako. Hiyo ndiyo ishara kwamba Mungu amekupa Roho Mtakatifu, hiyo ni kweli, na ameithibitisha imani uliyokuwa nayo ndani yako, na anatoa thibitisho lake kwa kukupa Roho Mtakatifu.

115 Basi kama unaye Roho Mtakatifu, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Kweli kabisa.

116 Kama akikana, mtu huyu anayezunguka kote kote, akisema, “Sasa, msiwasikilize watu hao. Ati mlishuka kwenye maskani moja hivi majuzi usiku?”

“Naam. Aa-ha.”

117 “Vema, sisi ni wafuasi wa *Fulani-fulani*. Hao si kitu ila kundi la makabwela.”

118 Hivi ulijua ya kwamba Paulo alimwambia Agripa, “Katika njia iitwayo ‘uzushi,’ hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu”? Mnajua uzushi ni nini? [Ndugu mmoja anasema, “Kichaa.”—Mh.] Naam. Hiyo ni kweli. Hivi wao hawakumwambia Yesu, “Sasa tunajua Wewe ni mwendawazimu”? *Mwendawazimu* linamaanisha “kichaa.” Mnaona?

119 “Njia inayoonekana ni ya kichaa.” Kwa sababu umepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Wewe si wa ulimwengu tena, bali umetengwa na ulimwengu. Unaona? Hivyo basi nia yako ni ya kiroho, nawe unayawazia mambo yaliyo Juu wala si mambo yanayoendelea hapa duniani. Upendo wako uko kwenye mambo yaliyo Juu.

120 Sasa, kama mtu huyu akikana kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

121 Sasa angalia. Utawasikia wakisema, “Loo, Yeye ni yeye yule.” Je, Yeye ni yule yule? Yeye ni yule yule? “Vema,” wao wanasema, “Yeye ni yule yule, kwa njia fulani.” Njia ipi? Mnaona? Njia ipi? “Vema, si—sijui. . . Ninaamini Yeye angali anaokoa.” Mnaona? Vipi kuhusu uponyaji? “Loo, la. Yeye hafanyi hivyo.”

122 Sasa, wakati alipokuwa hapa duniani, wao walisema, “Yeye anaweza kuponya, bali hawezi kuokoa.” Sasa wanasema, “Anaweza kuokoa, bali hawezi kuponya.” Mnaona, ni ibilisi tu, akichukua vinginevyo.

123 Lakini iwapo Yeye ni Yesu Kristo, kwa vyovyote vile, Yule aliyepakwa mafuta, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, Mponyaji yule yule, yeye yule.

124 Si wewe unayefanya miujiza. La. Wao wanataka kusema, “Hebu nikuone ukifanya jambo *hili*.” Sasa, Mungu kamwe hakusema niifanye. Tayari ameifanya. Jambo pekee ninalopaswa kufanya ni kulichukua Neno Lake na kulishikilia, na Yeye atalitimiza. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Sio wewe. Ni Mungu aliye ndani yako.

125 Kama vile Yesu alivyosema, “Sio Mimi nizifanyaye kazi; ni Baba Yangu aishiye ndani Yangu. Yeye huzifanya hizo kazi. Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kufanya chochote Mwenyewe; ila lile ambalo amwona Baba analitenda, hilo atenda Mwana vile vile.” Kwanza alitazama, apate kuona ono, yale Baba aliyomwambia. Yohana Mtakatifu, ninaamini, 5:19, mtasoma hilo, 5:19. Naam. Kama mtasoma, Yeye alisema, “Yale Baba anayonionyesha kufanya, hayo nafanya vile vile.”

126 Sasa tunaona, basi, kwamba ikiwa sisi—ikiwa sisi . . . kama akikana kwamba Yesu Kristo si yeye yule.

127 Kuna kitu kimoja tu ambacho Yeye hawezi kuwa, ambacho Yeye anaweza kuwa tofauti kwacho, hicho ni, mwili wa kawaida, wa nyama. Mnaona? Sasa, katika mwili wa kawaida, wa nyama, Mungu aliufufua huo kutoka kaburini, kwenye siku ya tatu, nao unaketi kwenye mkono wa kuume wa ukuu Wake huko Juu, kwenye . . . kwenye Kiti Chake cha Enzi. Yesu alishinda, akakichukua Kiti cha Enzi cha Mungu. Sisi tunaoshinda tutaketi pamoja na Yeye juu ya Kiti Chake cha Enzi, maana Kiti Chake cha Enzi ni kiti cha enzi cha Daudi, ambapo Yeye atatawala hapa duniani. Na sasa kwenye mkono wa kuume wa Mungu, mkono wa kulia wa nguvu na ukuu Wake, Yesu anatawala.

128 Sasa, Mle ndani, Yeye ni Kuhani Mkuu kutuombea juu ya maungamo yetu, tunapolikubali Neno Lake, tunaliamini Hilo moyoni mwetu, tunalipokea mle ndani, wala hatughairi, bali tunaamini kabisa litatukia. Uzao wa kweli wa Ibrahimu utashikilia kwenye hilo Neno. Haidhuru inachukua muda gani, Yeye atalitimiza. Hakuna wimbi ndani yake, mahali popote. Yeye atalitimiza. Hiyo ni kweli.

129 Sasa, mbabaishaji atasema, “La. Hilo, hilo sivyo lilivyo.” Basi almuradi wanalikana agizo *Hili*, inaonyesha hawawezi kuonyesha . . . wao . . . agizo lao limetiwa muhuri. Hawawezi kukuonyesha, kwa sababu wanakana. Iwapo . . .

130 Basi kama a—afisa, ningesema, “Vema, hapa, mimi ni mkuu wa polisi wa Marekani. Ninajua mimi ni afisa mkuu, na hii *hapa* sheria inayosema afisa mkuu hana budi kubeba hati hii ya utambulisho, iliyotiwa muhuri kwa muhuri wa Marekani.”

131 Unasema, “Vema, hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya wakati fulani uliopita. Haitubidi kuwa nayo siku hizi.” Yeye ni mbabaishaji. Hakuna lingine. Hayuko sahihi. Yeye hajaagizwa. Yeye hajatumwa.

¹³² Naye mtu yeyote atakayekana, ya kwamba Yesu Kristo si yeye yule jana, leo, na hata milele; mtu yeyote atakayekana “ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” anajaribu kuendelea na karatasi fulani ya ukasisi pasipo na muhuri wa lile agizo. Hiyo ni kweli kabisa, sasa. Hakika ni kweli. Hawezi kutumwa na Mungu, kwa sababu yeye anakana ule muhuri wenyewe, ambao, thibitisho lenyewe la lile agizo analopaswa kuwa nalo.

Kama afisa fulani alisema, “Haikulazimu kuwa na muhuri huo.”

¹³³ Unao, wewe mwenyewe. “Huu *hapa*, katika kitabu kinachosema huna budi kuwa na muhuri huo. *Hapa*, ni sheria za Marekani, zinazosema kwamba afisa mkuu anapaswa kuubeba muhuri huu.” Na endapo hana muhuri huo, kabisa yeye si afisa mkuu. Usimpokee, kwa sababu yeye si afisa mkuu, maana sheria ya kile kitabu inasema hana budi kuubeba muhuri huo.

¹³⁴ Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao. *Zitafuatana* na hao!” Sio, “Zinapaswa kufuata; labda; baadhi yazo, zitafuata.” Ilisema, “Zitafuatana na hao waaminio.” Hilo ndilo thibitisho la lile agizo, kwamba walikuwa wametumwa. Amina. Ninapenda hilo. Linanifanyia vizuri kujua hilo. Naam, bwana. Kwa hiyo ninajua hilo ndilo agizo lililoingia moyoni mwangu, muhuri wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli.

¹³⁵ Ninajua, kila mwaminio ambaye kweli ni mwaminio, yeye humwona mtu anayezikana hizo nguvu zake: Biblia ilisema, “Katika siku za mwisho wangukuwa na mfano wa utauwa, nao wangukana nguvu zake. Hao nao mjiepushe nao. Msiwapokee, hata kidogo.” Kweli. Watakuwa na makanisa makubwa na madhehebu mazuri, na fahari kuu, na urembo mkuu, na kadhalika namna hiyo.

¹³⁶ Angalieni, hapa, hivi majuzi usiku, hapa chini katika Phoenix, kundi la hao wasichana wadogo, wavulana huko nje, wakifanya bugibugi hii mpya, vyovyote mnavyouta upuuzi huo huko nje, nao wakachukuliwa sana na roho yake mpaka walikuwa huko nje mitaani. Iliwabidi polisi kuwaokota. Wameshawishika sana chini ya nguvu za ibilisi, naam, halafu hilo linapendwa sana na watu.

¹³⁷ Lakini hebu mtu acheze katika Roho wakati mmoja, chini ya nguvu za Roho Mtakatifu! Hiyo ni kweli. Jambo ndilo hilo. “Ishara za Mungu zitafuatana na hao waaminio.” Naam.

¹³⁸ Hawezi—hawezi kusema ametumwa kutoka kwa Mungu, kisha alikane agizo Lake. Hebu tuangalie baadhi ya wale ambao Mungu aliwatuma, tuone kama Yeye sikuzote aliwatambulisha waaminio Wake. Sasa angalieni.

¹³⁹ Hebu tumchukue Musa. Musa alikuwa na wito maishani mwake, hiyo ni kweli, bali kamwe hakutumwa. Alidhani alitumwa, basi angalieni jinsi alivyoshindwa vibaya. Lakini wakati Mungu alipomtuma kutoka kwenye kichaka kilichowaka

moto. . . Wakati alipokuwa huko nje mbele ya seminari ya Farao, yeye alitoka na hati zake za utambulisho. Zisingefanya kazi. Mungu asingezitambua.

¹⁴⁰ Angalia, alishuka kule na kumwua mtu bila kuagizwa kufanya hivyo, ndipo ikambidi kuitoroka Misri. Naye akashuka kule chini na kulizamisha jeshi zima la Misri, akiwa na agizo la kufanya hivyo, na hakuna neno lililosemwa juu yake. Hiyo ndiyo tofauti yake. Kamwua mtu mmoja ikamlazimu kutoroka. Loo, jinsi alivyokuwa katika hali mbaya, maana alifanya hivyo bila agizo. Bali alishuka akaenda kule pamoja na agizo, akalizamisha jeshi zima, akajipatia utukufu kwa Mungu kwa ajili Yake. Mnaona?

¹⁴¹ Jinsi Mungu anavyowafanya watu wafanye mambo ya kuchekesha! Maskini mzee huyo, muungwana sasa, alitoka kule akiwa na kila namna ya shahada za chuoni. Lakini, na, loo, asingewazia juu yake, hapa kwenye umri wa miaka themanini. Basi kesho yake asubuhi, huyu hapa anaelekea Misri, huku mke wake ameketi akimtagaa nyumbu, akiwa na mtoto wake nyongani mwake, akisafiri, maskini masharubu makubwa yakipeperushwa namna *hiyo*, na fimbo iliyopinda mkononi mwake.

“Kwani unaenda wapi, Musa?”

¹⁴² “Ninashuka kwenda Misri, kuiteka.” Uvamizi wa mtu mmoja. Kwa nini? Jambo ni kwamba, yeye aliiteka. Kweli. Kama vile mtu mmoja kwenda kule kuiteka Urusi nzima. Ilikuwa ni kitu gani? Yeye alikimbia. . . Hapo alipokuwa afisa wa daraja la juu, afisa wa daraja la juu sana lililokuwako, wa pili kutoka kwa Farao huko Misri, aliitoroka Misri kwa sababu hakuwa na agizo la kuwakomboa wana wa Israeli. Lakini basi anarudi, akiwa ni mtu mmoja dhidi ya kitu hicho chote, pamoja na lile agizo, naye akaiteka. Kwa nini? Alikuwa na agizo, naye alikuwa na thibitisho lake. Angeweza kuthibitisha kwamba Mungu alikuwa amemtuma. Amina.

“Utafanya hivyo na kitu gani, Musa?”

“Maskini fimbo hii iliyopinda niliyo nayo mkononi mwangu.”

“Ati kwenda kufanya nini?”

“Hili ni agizo langu.”

“Ati nini?”

¹⁴³ “Mungu amenipa ishara mbili za kufanya mbele zao. Jambo ndilo hilo. Aliniambia niende nifanye hivi. Kasema, ‘Ishara hizi zitafuata,’ kama nikishuka kwenda kule. ‘Itupe chini mbele za Farao, uone kitakachotukia. Itageuka kuwa nyoka. Kisha useme, “BWANA ASEMA HIVI, Farao, waache watu Wangu waende zao.”’”

¹⁴⁴ Musa akashuka kule na kuitupa chini. Wale waganga wakaja hapo, wakafanya jambo lile lile. Kisha Mungu akalithibitisha agizo lake. Nyoka wake akawala hao wengine.

¹⁴⁵ Hivi uliwahi kuwazia, “Hao nyoka walienda wapi?” Walienda wapi? Ilikuwaje kwa hizo fimbo? Zote zilikuwa katika fimbo moja. Mnaona? Yeye alizila, nyoka wa Musa. Kwa sababu, ilikuwa ni nini? Thibitisho. Amina. Haleluya! Alipata thibitisho la agizo lake. Akalitekeleza. Akawatoa watoto, nayo Bahari ya Shamu ikamzuia kisha ikaondoka njiani.

¹⁴⁶ Kwa nini? Alikuwa na agizo na thibitisho lake. Mungu alikuwa pamoja naye, na akafanya ishara na maaajabu.

¹⁴⁷ Lakini, ambapo, kama mtu akiagizwa na Mungu wa kimbinguni, nguvu za kimbinguni za Mungu zitakuwa pamoja na agizo hilo la kimbinguni. Sio yale unayojifunza katika Ph.D. na LL.D. na aljebra, na mambo haya yote. Hizo huthibitisha sarufi yako nzuri na hotuba mimbarani wakati unaposema “ah-mena” kama ndama. Lakini hebu nikwambie jambo fulani. Lakini unapopata thibitisho la agizo la Mungu, ulilopewa na Roho Mtakatifu, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Samahani kwa tamshi hilo.

¹⁴⁸ Thibitisho. Mungu alithibitisha, kwa sababu Yeye alikuwa ni Mungu wa kimbinguni, aliyetoa nguvu za kimbinguni, kwa ajili ya ukombozi wa kimbinguni. Ninaliamini.

¹⁴⁹ Mungu siku hizi hatawakomboa watu Wake kwa elimu. Kamwe hakuahidi kufanya hivyo. Hatawakomboa kwa thiolojia. Kamwe hakuahidi kufanya hivyo. Hatawakomboa kwa sayansi. Kamwe hakuahidi kufanya hivyo. Hatawakomboa kwa dhehebu. Kamwe hakuahidi kufanya hivyo. Bali Yeye atawakomboa kwa nguvu, nguvu za kimbinguni, za kuyabadilisha maisha yao na kuwafinyanga wakawa watoto wa Mungu. Amina.

¹⁵⁰ Musa alikuwa na agizo. Alikuwa na ishara za kulithibitisha agizo lake.

Sasa, Yesu, vivyo hivyo, alisema, “Ishara hizi!”

¹⁵¹ Musa alisema, “Niwaambie nini? Nitawaambiaje kwamba Mungu wa baba zao amenituma?”

Kasema, “Una nini mkononi mwako?”

Kasema, “Fimbo.”

¹⁵² Akasema, “Itupe chini. Weka mkono wako kifuni mwako, utoke. Wahubirie uponyaji wa Kiungu.” Hilo ni thibitisho. Hakika. “Nitakupa ishara mbili.”

¹⁵³ Sasa, Mungu yuyo huyo hawezi kubadilika. Wakati alipolituma kanisa Lake, kuwakomboa watu kutoka kwenye utumwa huu wa kijehanamu wa Misri ambapo mambo haya yote yamewaingiza watu siku hizi, Yeye alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Usiogope kuliweka Neno hilo

huko nje, kwa sababu ni Kweli. Ni Neno la Mungu. Usiache ibilisi alielezee Hilo vibaya kwako; kwa sababu si halali. Yeye hulitimiza Neno Lake. Sasa, ninaamini hilo kwa yote yaliyo ndani yangu.

¹⁵⁴ Eliya alitumwa huko chini. Ninaweza kumwona asubuhi hiyo. Ninawazia yeye na Yezebeli walikuwa na ugomvi kwelikweli. Lakini huyu hapa siku hiyo akishuka chini, jamaa mdogo mwenye upara, na masharubu yakining'inia, akishuka asubuhi hiyo, ameshika barabara hiyo akienda zake Samaria. Macho hayo yameelekezwa mbinguni; tabasamu usoni mwake. Maskini ile fimbo ikiigonga barabara. Lakini, ndugu, yeye alikuwa na "BWANA ASEMA HIVI."

¹⁵⁵ "BWANA ASEMA HIVI." Akaenda moja kwa moja mbele ya uso wa rais ama wa mfalme, kasema, "Hata umande hautashuka kutoka mbinguni mpaka nitakapouagiza." Ilikuwa ni kitu gani? Alikuwa na agizo. Ilinyesha kesho yake? La. Alikuwa na thibitisho la hiyo. Mnaona?

¹⁵⁶ Akasema, "Kwea kule, Eliya, ukaketi chini. Nimeagiza uwe na wapagazi na watumshi waje wakakulishe." Kwa hiyo kunguru wakamlisha.

¹⁵⁷ Ndipo wakati akiwa juu mlimani kule siku moja, "Loo," mfalme akasema, "hakuna kitu kwa jamaa huyo. Nitawatuma watu hamsini. Siamini yeye ni kitu ila maskini mzee mlokole. Hivi hatukumjua huku, akizungumza juu ya Yezebeli, mke wangu, kujipaka rangi na kila kitu namna hiyo, akizungumza juu ya maisha haya yote ya kisasa?"

¹⁵⁸ Na kuishi kwa mfano wa mama taifa, kama vile wengi wetu sisi Wapentekoste tufanyavyo! Naam. Hiyo ni kweli. Wanawake wetu wa Kipentekoste, hiyo mitindo mikuu ya kukata nywele kichwa-maji, na vitu kama hivyo, ndiyo, naam, wakijipaka rangi, kujipodoa, kuvaa kaptura. Nayo Biblia ilisema, "Ni chukizo machoni pa Mungu." Mnawezaje kufanya hivyo? Hiyo ni kweli. Mbona, mwajua, kama ukidai, dada, wewe, kitu fulani kimeanguka, kama unaweza kuzikata nywele, huku Biblia inasema...

¹⁵⁹ Sasa, wengi wenu wanawake wa Kipentekoste hamtajipodoa. Hakuna kitu katika Biblia kuhusu hilo. Lakini basi mtazikata nywele zenu. Nayo Biblia ilisema, ya kwamba, "Mwanamke anayezikata nywele zake ni aibu." Hiyo ni kweli.

¹⁶⁰ Nanyi mtavaa kaptura, ama maskini hizi...Ni nini... Mnaona? Chochote kile, zinaonekana kama nguo za mwanamume. Nayo Biblia ilisema, ya kwamba, mwanamke yeyote atakayevaa nguo namna hiyo, "Ni chukizo mbele za Mungu." Kwa maneno mengine, "Ina—inavunda, kwa Mungu. Inaonekana mbaya." Halafu kama unaye Roho Mtakatifu ndani yako, ambaye ni Mungu, mnawezaje kuzivaa na bado

mdai mnaye Roho Mtakatifu? Mbona, maisha yenu wenyewe yanathibitisha mna kasoro. Hiyo ni kweli.

¹⁶¹ Ninajua hilo linaunguza, bali ni—ninawaambia kuna shida gani usiku wa leo. Tunahitaji kuunguzwa zaidi ndiko wanakohitaji, kucharazwa zaidi. Hiyo ni kweli. Ndiyo shida, tuliachilia mambo hayo. Ndugu, hebu niwaambie, hamna budi kujifunza ABC zenu kabla hamjaenda mbele zaidi, mnaona, hiyo ni kweli kabisa, sikuzote kuamini ya kwamba Neno la Mungu ni kweli. Haijalishi ni kitu gani, linganisha tu na Hilo. Naam, bwana.

¹⁶² Eliya akiketi juu ya mlima kule, naye Mungu akasema, “Sasa, hutasumbuliwa.” Kasema, “Nitakutuma kule juu mpaka watu hao watakapotubu.”

¹⁶³ “Loo,” Ahabu akasema, “si lazima tufanye toba yoyote. Maskini mzee yule mlokole, hajui analozungumzia. Ni mmoja wa hao watakatifu wanaojibingirisha. Tunaninii tu. . . Nipe watu hamsini hodari sana. ‘Kweeni kule mkamshushe maskini mzee yule mlokole.’”

¹⁶⁴ Ninaweza kumwona afisa yule aliyepandishwa cheo akisema, “Naam, bwana. Ninalo agizo lako, bwana. Nitamrudisha moja kwa moja.”

¹⁶⁵ Huyu hapa anakuja, akitembea taratibu, chu—chuma kikigonga chini, panga hizi kubwa na mikuki, na watu hamsini hodari wa walinzi wa Ahabu wakakwea kilima namna hiyo.

Huyo hapo Eliya ameketi katika jua kali, akiangalia kote namna *hiyo*.

¹⁶⁶ Wao wakasema, “Hei! Tunakutafuta, jamani. Tuna hati zetu za utambulisho hapa. Sisi ni walinzi wa Ahabu. Tunakutafuta. Tutakurudisha.”

¹⁶⁷ Akasimama, kasema, “Naam, nina hati za utambulisho, pia. Kama mimi ni mtu wa Mungu, moto na ushuke kutoka mbinguni.” Ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni thibitisho. Naam, bwana.

¹⁶⁸ Juu ya Mlima Kameli, wakati alipokuwa na shindano la kuamua kati ya miungu wa uongo na Mungu wa kweli. Yeye aliweka dhabihu nje, akaenda huko nje, na kusema, “Bwana Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Israeli, na ijulikane leo kwamba Wewe ni Mungu katika Israeli, nami ni mtumishi Wako, na nimefanya haya yote kwa amri Yako.”

¹⁶⁹ “Nikalihubiri Neno,” kwa amri Yako, Bwana, “ulimwenguni mwote, kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Amri Yako.

¹⁷⁰ “Sasa, Bwana, na ijulikane ya kwamba Wewe uliniambia nifanye jambo hili. Uliniagiza kufanya jambo hili, sasa lithibitishe, Bwana.” Basi yapata wakati huo, moto ukashuka

kutoka mbinguni. Lilikuwa ni thibitisho lake. Yeye alikuwa pamoja na Neno. Mnaona?

¹⁷¹ Mungu sikuzote hulithibitisha Neno Lake. Yeye, Yeye hutoa thibitisho la Neno Lake. Sasa, tunajua ya kwamba hiyo ni kweli. Loo, ni mara ngapi, hilo! Tunao watu mbalimbali hapa ambao tungewaendea moja kwa moja. Bali kuokoa wakati. . .

¹⁷² Yesu, hapo alipokuja duniani, nao wakasema, “Yeye, akiwa ni Mwanadamu, anajifanya Mwenyewe Mungu? Loo, jamani! Vema, tunajua Yeye alikuwa ni nani. Alizaliwa mtoto haramu. Mbona, Yeye hata haninii. . . Tunamjua mama Yake, Mariamu, na Yusufu. Walimpata mtoto huyo kab- . . .”

¹⁷³ Yesu akasema, “Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Hivi hamwamini kwamba Mimi ni Masihi? Kazi nizifanyazo Mimi zinathibitisha yale ninayodai. Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiamini. Lakini kama nikizitenda kazi za Baba Yangu, basi ziaminini hizo kazi, hata kama hamwezi kuniamini Mimi.” Hilo lilikuwa ni thibitisho. Hilo liliwafaa nini? Hakika. Kasema. . .

¹⁷⁴ Mungu, ambaye Mungu anamtuma, Mungu humlinda. Mungu hulithibitisha Neno. Kama Mungu alimtuma balozi mahali fulani, kufanya jambo fulani, Yeye hana budi kusimama nyuma ya agizo hilo. Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁷⁵ Alisema, “Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msi—msiniamini Mimi, lakini,” kasema, “kazi zenyewe nizifanyazo Mimi zinalithibitisha agizo Langu.” Amina. Hilo liliwacharaza kwelikweli. Sivyo? “Kazi nizifanyazo Mimi.” Naam. Naam, bwana. “Kama hufanyi hivyo, kama hamwezi kuamini kwamba nilituma na Mungu, basi jambo mnalopaswa kufanya ni kuziamini hizo, kazi nizifanyazo, ama, hebu nikuone ukifanya kazi zile zile,” hizo hapo, “ikiwa hamniamini Mimi.” Ni. . . Loo, jamani!

Kuna baadhi yao waliomwamini Yeye.

¹⁷⁶ Wakati yule mwanamke kisimani alipoiona ishara Yake ya Kimasihi, yeye alisema, “Tunajua Masihi hufanya hivyo.” Akaenda akawaambia watu, kasema, “Njoni, mwone Yule niliyempata, Mtu aliyeniambia siri hasa za moyo wangu. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?”

¹⁷⁷ Maskini Nathanaeli, wakati aliporudi pamoja na Filipo, naye Yesu. . . akaja Mbele za Yesu, naye Yesu akasema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

¹⁷⁸ Sasa, yeye alikuwa mtu aliyefunzwa, maana alilijua Neno. Yeye alijua Masihi angekuwa Mungu-nabii. Kwa hiyo walijua Musa alikuwa amesema hilo. “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea nabii.” Yeye alijua pia, ya kwamba Mungu alisema, “Akiwepo mtu miongoni mwenu, aliye wa kiroho ama nabii, Mimi, Bwana, nitamthibitisha. Nitaninii. . . Asemayo,

yakitimia, basi aminini.” Mnaona? Walitaka kutafuta kujua kama Yeye alikuwa hivyo. Walijua kulipaswa kuwe na nabii atakayeinuka kwenye wakati kama huo, nao walitaka kujua Yeye alikuwa ni Nani.

¹⁷⁹ Kwa hiyo akaenda mbele za Filipino, naye Filipino akamwambia la kufanya. Ama, Filipino akampeleka Mbele za Yesu, hasa.

¹⁸⁰ Ndipo alipoenda mbele za Yesu, Yesu alisema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

“Ulinijua je Wewe, Rabi?”

¹⁸¹ Kasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.”

¹⁸² Akasema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu.” Hizo hapo hati Zake za utambulisho.

¹⁸³ Mwanamke kisimani, wakati alipomkuta amesimama pale kisimani, Yeye alisema, “Nipe maji ninywe.”

¹⁸⁴ Akasema, “Si desturi. Wewe unakiuka sana desturi ze—ze—zetu hapa. Tuna ubaguzi. Sisi Wayahudi na Wasamaria hatuna ushirikiano sisi kwa sisi. Wewe ukiwa ni mwanamume, Myahudi, nami ni mwanamke Msamaria, imekuwaje kwamba Wewe waniomba fadhila, nikupe maji unywe?”

¹⁸⁵ Akasema, “Mwanamke, kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe.”

¹⁸⁶ Naye akasema, “Mbona, kisima ni kirefu. Huna kitu cha kuchotea.”

Akasema, “Maji nitoayo hayamo katika kisima hicho.”

¹⁸⁷ Mazungumzo yakaendelea, yakaendelea mbele, kwa muda kidogo, mnaona, mpaka Yeye, anachojaribu kufanya: Kuwasiliana na roho yake, ndipo akapata mahali shida yake ilipokuwa. Kasema, “Nenda kamwite mume wako mje naye hapa.” Anamtaka yeye, ajue kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Kasema, “Nenda, kamwite mume wako mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

¹⁸⁸ Kasema, “Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, naye yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

¹⁸⁹ Akasema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii.” Kasema, “Tunajua ajapo Masihi Yeye atafanya mambo hayo.”

Yeye akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

¹⁹⁰ Akaingia mjini. Alithibitishiwa. Akaingia mjini na kusema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi? Hilo si ni thibitisho kwamba Ndiye?”

¹⁹¹ Yesu akasema, “Kazi zenyewe nizifanyazo Mimi zinalithibitisha agizo Langu.” Hiyo ni kweli. Mungu alimtuma. Alikuwa awe ni Nabii huyo.

¹⁹² Mwajua, walimwambia Yohana, “Wewe ni Eliya? Wewe—wewe ni mmoja wa wale manabii? Wewe ndiye yule Nabii aliyekuwa aje?”

¹⁹³ Yohana akasema, “Mimi siye. Lakini Yeye amesimama miongoni mweni, mahali fulani. Yeye atajithibitisha Mwenyewe atakapokuja, maana Mungu atamthibitisha.” Hiyo ni kweli kabisa. Kama mtu ametumwa na Mungu, Mungu anawajibika kumthibitisha mtu huyo, hiyo ni kweli kabisa, kwamba ametumwa. Loo, naam, thibitisho.

¹⁹⁴ Yule mtu aliyezaliwa kipofu, alikuwa na ushuhuda wa kushawishi kabisa kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Sasa, maskini mtu huyo, hakuninii—hakuninii... Wakati hao wanathiolojia wote walipomshika kwenye umati huko juu, na kusema, “Aisee, tunajua ya kwamba ulizaliwa kipofu.” Kasema, “Tunajua ya kwamba—ya kwamba hukuwa na mboni za macho, hata kwenye hayo matundu.” Kasema, “Tunajua ulizaliwa kipofu.” Akasema, “Ni nani aliyekuponya?”

¹⁹⁵ Naye akasema, “Huyo Mtu aliniambia ya kwamba nimeponywa.” Kasema, “Ninajua kwamba Yeye aliniponya.” Kasema, “Na—na—najua hilo.”

¹⁹⁶ Kasema, “Vema, sasa, Mtu huyo ni mwenye dhambi. Tunajua Yeye ni mwenye dhambi, kwa sababu hakujiunga na dhehebu letu. Hakuja kwa njia yetu. Yeye hafundishi fundisho letu. Anatupinga.” Kasema, “Sisi, tunajua ya kwamba Yeye hawezi kuwa ni wa Mungu. Tunajua ya kwamba ana kasoro, kwa sababu hakukubaliana nasi.” Kasema, “Mtu huyo ni mwenye dhambi.”

¹⁹⁷ Sasa, maskini kipofu huyu asingeweza kubishania hoja hiyo. Yeye hakuwa mwanathiolojia. Yeye, asingeweza kubishania hiyo hoja. Alisema, “Sasa...” Lakini alikuwa na majadiliano ya kushawishi sana pia. Akasema, “Kama Yeye ni mwenye dhambi, ama si mwenye dhambi, sijui mimi. Bali jambo hili moja nalijua,” amina, “ambapo nilikuwa kipofu, sasa ninaona.”

¹⁹⁸ Nimewasikia watu wakisema Hili lilikuwa ni kundi la watu wenye kichaa. Nilikuwa na watu walioniambia, nilipompokea Roho Mtakatifu, ya kwamba nilirukwa na akili. Vema, kama hiyo ni kweli, ama si kweli, sijui mimi. Lakini lipo jambo moja nijualo: ambapo wakati mmoja nilikuwa ni mwenye dhambi, sasa nimeokoka. Hiyo ni kweli. Ambapo wakati mmoja nilikuwa nimepotea, sasa nimepatikana. Unaweza kuliita ulokole, lolote utakalo, bali ni thibitisho kwangu ya kwamba Yeye angali ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli. Naam.

¹⁹⁹ Yeye—yeye—yeye alikuwa na thibitisho. Alikuwa na hotuba ya kushawishi mno kwamba Yeye alikuwa... Yeye—Yeye alikuwa... kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, kwa sababu Yeye alifanya mboni za macho katika mtu asiye kuwa na mboni za macho. Naam, bwana. Kwa maneno mengine, yule

kipofu angeweza kusema, “Nimekuwa nikija kanisani mwenu wakati huu wote. Sioni kitu kama hicho kikitendeka huku. Basi kama Yeye aliumba mboni za macho, hakuna Mwumbaji ila Mungu. Ingetoka wapi? Hebu tuwaone mkilifanya. Hebu tuone jinsi mnavyolifanya.”

²⁰⁰ Iliwabidi kunyamaza. Hao wakizungumza juu ya Mungu wa kimbingni, yule Muumba mkuu wa mbingu na nchi, wala wasingeweza kuumba uhai mzuri. Mnaona? Haya basi. Wasingeweza kuumba chochote.

²⁰¹ Lakini huyu hapa Yesu anakuja na kuweka mboni za macho katika mtu asiye kuwa na mboni za macho, aliyezaliwa kipofu. Ninawaambia, hilo linashawishi. Thibitisho la pudini ni kuila. Hiyo ni kweli kabisa. Kwa hiyo alikuwa na thibitisho kwamba Yeye alikuwa hivyo. Hiyo ni kweli.

²⁰² Ninawazia Paulo, huko nje usiku huo, wakati siku kumi na nne mchana na usiku, bila ya mwezi, nyota, wala chochote kile, huko nje kwenye hiyo bahari; maskini jamaa huyo mdogo akiikokota minyororo hiyo kwenye staha la meli hiyo iliyojaa maji, nayo ikiwa karibu kuzama. Walikuwa wametupa chakula chote na kadhalika, na hao mabaharia hawakuwa wamekula kwa siku kadhaa. Naye huku anaikokota hiyo minyororo, akinena habari za Yesu ambaye aliishi wakati mmoja, akinena kuhusu Yesu aliyesulubishwa.

²⁰³ Nawazia hao askari na mabaharia walisema, “Loo, jamani, nyamazeni!”

²⁰⁴ Akaendelea tu kutembea kote, akisema, “Lakini, mwajua, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele,” akitembea tu, kwenye staha, huku akiikokota minyororo hii.

²⁰⁵ Kasema, “Angalieni jamaa aliyefungwa minyororo, jamaa anayeenda kule kwa Kaisari, kule Rumi, akahukumiwe. Huyu mtu hana budi kufa, halafu anazungumzia kitu fulani kuhusu dini. Loo, nyamaza!”

²⁰⁶ Nao wakaendelea kukokota. Lakini, usiku mmoja, wakati matumaini yote yamekwisha! Loo, jamani.

²⁰⁷ Kila wakati radi ilipomulika, wimbi fulani, pepo elfu kumi waliketi juu ya hizo bahari, kasema, “Tumekupata sasa, Paulo. Loo, wewe utalighairi.”

²⁰⁸ “La, bwana. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli. Ninajua Yeye aliniambia niende Rumi.”

²⁰⁹ Huyu hapa, akiyumbayumba, meli karibu kuzama. Wazieni tu, jua, mwezi, au nyota hazikuwa zimewaka kwa muda wa siku kumi na tano, ama kumi na nne. Hiyo ni hali mbaya; meli ya kale iliyojaa maji, na kitu hicho karibu kizame, kila kitu namna hiyo.

²¹⁰ Yeye alikuwa amesimama kwenye mtumbwi mtupu, usiku mmoja, akiomba, hapana shaka, ndipo likatokea ono. Malaika

wa Bwana akamtokea, kasema, “Usiogope, Sauli. Kila kitu ni sawa.”

²¹¹ Huyu hapa anakuja, akikimbia, akiwa na agizo, akiitikisa minyororo hiyo, akisema, “Iweni hodari. Iweni na imani nzuri, kwa maana Mungu ninayemtumikia alimtuma Malaika Wake jana usiku. Niliona ono, na Yeye akaniambia nisiogope, kwa kuwa hakutakuwako na uhai utakaopotea kwenye meli hii. Basi, ndugu zangu, kuleni chakula kidogo, na mshangilie tu. Kila kitu ni shwari.”

²¹² Ningewazia walijisikia kigeni sana. Bali walipoona maskini meli ile imetulia mahali pa usalama huko ng’ambo, ilithibitisha kwamba Paulo alikuwa ametumwa kutoka kwa Mungu na alijua aliyokuwa akizungumzia. Mungu alilithibitisha.

²¹³ “Akiwepo mmoja miongoni mwenu aliye nabii, na yale asemayo yanatimia, basi msikieni, kwa sababu Mimi niko pamoja naye.” Hiyo ni kweli.

²¹⁴ Wakati, wenyeji wa kisiwa hiki, wanakisiwa, walipomwona akiokota kuni, nao wakasema, “Hapana budi yule ni mwuaji katili sana, minyororo hiyo yote juu yake.”

²¹⁵ Maskini Paulo, karibu agande, nayo mavazi yake yote yamelowa maji, alikuja huku na kuokota lundo la kuni, akaanza kuzitia motoni. Na nyoka aliyemuuma mkononi angalimwua, jamani, katika dakika moja. Paulo akamwangalia, namna *hiyo*, na kusema, “Mungu, Wewe uliniambia nilipaswa kwenda Rumi bado.” Akamtikisa motoni, kisha akarudi kuokota kuni zingine.

Kasema, “Hebu mwangalieni akianguka afe.”

²¹⁶ Dakika chache, wakalibadilisha. Kwa nini? Agizo lake lilikuwa limethibitishwa. Wao wakasema, “Yeye ni mungu aliyeshuka kutoka mbinguni.” Kweli.

²¹⁷ Alikuwa na thibitisho, maana Yesu alisema, “Watavikanyaga vichwa vya nyoka na nge, wala hakuna kitakachowadhuru.” Naam, bwana. Alikuwa na—alikuwa na—na ushahidi wa kulithibitisha.

²¹⁸ Sasa sina budi kuharakisha, enyi marafiki. Ningekaa hapa pamoja nanyi usiku kucha namna hiyo. Lakini mambo mengine machache tu.

²¹⁹ Sasa, nabii alisema, “Itakuja siku isiyoweza kuitwa mchana wala usiku, siku yenye ukungu, mavunde, utusitusi, lakini,” kasema, “wakati wa jioni itakuwa Nuru.” Hiyo ni kweli.

²²⁰ Jua huchomoza mashariki, na kutua magharibi: j-u-a. Ustaarabu umesafiri kutoka mashariki kwenda magharibi. Bali wakati M-w-a-n-a alipochomoza, ile Nuru iliwashukia watu wa mashariki.

²²¹ Sasa tumekuwa na siku za shirika, madhehebu, na watu wakimkubali Kristo, nao walikuwa na Nuru ya kutosha

wanaweza kujua ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu. Nao wakatembea katika hiyo Nuru, na kadhalika. Wamejenga makanisa, na makanisa mazuri ya jimbo, na shule, na kadhalika. Hilo limekuwa ni sawa.

²²² Lakini, kumbukeni, iliahidiwa ya kwamba mawingu yote yangeondoka wakati wa jioni. Ni wakati wa jioni sasa. Basi wakati mawingu yote yameondoka, Mwana yule yule, M-w-a-n-a, aliyeziwasha nguvu Zake kupitia Roho Mtakatifu juu ya watu wa mashariki, ameninii, katika miaka hamsini iliyopita, ameyavunja mawingu ya madhehebu na kila kitu, na kummwaga Roho Mtakatifu juu ya watu wa magharibi. Huyu, Mwana yule yule, Roho Mtakatifu yule yule, ishara ile ile, Nuru zile zile, nguvu zile zile, thibitisho lile lile, kila kitu ni vile vile kilivyokuwa. Nayo Injili imehubiriwa kwa nguvu na dhihirisho, mahali popote katika nchi nyingi. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Kote ulimwenguni, ishara na maaajabu zinawafuata waaminio.

²²³ Hapa, miaka michache iliyopita, wao walisema, “Lile kundi,” kasema, “mbona, kamwe hamtaweza.” Kasema, “Kamwe hawataweza kulieneza kote.” Kasema, “Wao ni kundi dogo tu kule chini m—mtaani mahali fulani, wakiwa na sufuria ya bati mahali fulani, wakipiga tari ndogo.”

²²⁴ Lakini, ndugu, ujumbe huo, pamoja na watu wenye mioyo iliyo na njaa waliotoa chakula cha watoto wao, na kila kitu kingine, nao wamewadhamini hao wamishenari, mpaka ukaenda kutoka mashariki, magharibi, kaskazini, kusini. Taifa lolote unaloingia, kunayo mioto ya kipentekoste inayowaka kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

²²⁵ Nimeingia ndani sana misituni, hata watu hawajui mkono wa kulia wala wa kushoto. Hawakumjua Mungu zaidi ya sanamu fulani huko nje. Hiyo ni kweli. Ningesimama kule na kulielezea Neno kikamilifu kabisa. Ndipo Roho Mtakatifu akafanya ishara na kuonyesha, kuwaambia watu kwamba wao ni nani, siri za mioyo yao, nikawaonyesha kwamba Yesu alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.”

²²⁶ “Mtu huyu, sijui jina lake, bali nitaendeleza herufi zake, nawe ulifasiri kwangu.” Ingenibidi kuendeleza herufi zake labda kiasi *hicho*, kulitoa namna *hiyo*.

“Amina. Hiyo ni kweli.” Wangeketi chini na kutazama.

²²⁷ Niseme, “Sasa, Yesu alisema, ‘Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.’ Hii ilikuwa ndiyo ishara Yake ya Kimasihi.”

²²⁸ Naye Yesu amekaribia sana kuja duniani sasa, mpaka nguvu Zake zimeanza kuwashika watu, na kumalizia, kuwafanya tayari kwa ajili ya Bibi-arusi, kuwafanya tayari wapate kutwaliwa juu katika ule Unyakuo, Kanisa ambalo litaenea kikamilifu hasa, lipate kutwaliwa juu. Kupitia nguvu Zake, atawavuta hao wengine wote waliozaliwa mara ya pili, kutoka duniani. Yesu yuaja.

229 Kama vile mkono wangu utakavyofanya kivuli ukutani, zaidi, kivuli hicho kinaendelea kuwa kizito zaidi na zaidi na zaidi, kadiri mkono wangu unavyokaribia, halafu baada ya kitambo kidogo hicho kivuli na mkono wangu vinakuwa mmoja.

230 Nalo kanisa lilianza kwenye wakati wa Martin Luther, chini ya kuhesabiwa haki; chini ya Wesley, kupitia utakaso; na sasa katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, pamoja na Wapentekoste, kule kurudishwa kwa karama. Na kutoka kwa hao Wapentekoste Yeye anawavuta masalio *hapa* juu, kumwonyesha Yesu Kristo, kuuakisi Uzima Wake yeye yule tu jana, leo, na hata milele, hasa, wakati Nuru za jioni zinapoangaza. Hiyo ni kweli kabisa.

231 Angalieni, moja kwa moja kwenye ishara ya kisayansi, tunayo moja kwa moja katika Washington, DC, Nguzo ile ile ya Moto. Ni wangapi wamepata kuiona Hiyo, hizi Nuru? Hakika. Kila mahali. Mnaona? Mnaona? Nguzo ile ile ya Moto iliyokutana na Paulo, akienda zake Dameski. Yesu, wakati Yeye alipokuwa duniani. . .

232 Mtu yeyote anajua ya kwamba Kristo huyo, ile—ile Nguzo ya Moto, yule Malaika wa Bwana aliyewatoa Israel Misri, akawaingiza kwenye nchi ya ahadi, alikuwa ni Malaika wa agano. Mtu yeyote anajua hilo. Hakika. Vema, huyo alikuwa ni Kristo.

233 Kwa sababu, Biblia ilisema, ya kwamba, “Musa alichagua kushutumiwa kwa Kristo kwamba ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri.” Naye akaenda pamoja na Kristo, kabla hajafanyika mwili, naye akaifuata hiyo Nuru.

234 Yesu, alipokuwa duniani, Yeye alisema, “Nimetoka kwa Mungu, nami naenda kwa Mungu.” Walimsulubisha. Yeye alikuwa ni Mwokozi aliyekufa kwa ajili ya dhambi zetu, naye akamzika. Akafufuka na kupaa Juu.

235 Basi miezi michache baada ya hapo, Paulo alikuwa akienda zake Dameski, naye akapigwa akaangushwa na Nuru. Kundi la askari likiwa pamoja naye, hakuna mmoja wao aliyeiona Hiyo. Hakuna mmoja wao aliyemwona Huyu ila Paulo. Lakini ilikuwa—ilikuwa dhahiri sana kwake, hata ikayapofusha macho yake. Alikuwa kipofu kwa muda. Naye akaangalia huko juu, nayo hiyo Nguzo kuu ya moto imening’inia mbele zake, ndipo Yeye akasema, “Sauli, Sauli, mbona unanitesa?”

Akasema, “U nani Wewe, Bwana?”

236 Yeye akasema, “Mimi ni Yesu, na ni vigumu kwako kupiga teke michokoo.”

237 Sasa, Roho Mtakatifu yuyo huyo, tunamwona moja kwa moja miongoni mwa wapentekoste leo hii, Nuru ya jioni, moja kwa moja miongoni mwa wapentekoste. Kitu gani? Wakihubiri Injili ile ile, akitoa thibitisho la Injili ile ile. Ishara zile zile zilizofuata kule ndizo ishara zile zile zinazofuata sasa.

²³⁸ Na kama Nguzo hiyo ya Moto, ama Nuru, tuliyo nayo pamoja nasi, haikutoa Roho yule yule na ushahidi ule ule ambao ilitoa wakati ilipokuwa ndani ya Yesu Kristo, basi ingekuwa ni nguzo nyingine ya moto, roho mwingine, ingekuwa ni kitu kingine. Lakini kama kweli inatoa na kufanya vile hasa Yesu alivyofanya, wakati aliposema ninii. . . “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Kweli.

²³⁹ “Nyingi kuliko hizi atafanya, kwa kuwa naenda kwa Baba.” Ya King James ina “kubwa,” bali angalieni kwenye ile ya asili, inasema “zaidi.” Usingeweza kufanya kubwa zaidi. Aliwafufua wafu, na kuyakomesha maumbile, na kila kitu. Lakini Yeye angefanya nyingi zaidi, kwa sababu Roho Mtakatifu hakuwa katika Mtu mmoja pekee, Kristo, Mwana wa Mungu, Yeye alikuwa katika Kanisa la ulimwenguni mwote. “Nyingi kuliko hizi mtafanya, maana naenda kwa Baba Yangu.” Loo, jamani!

²⁴⁰ Huduma Yake ile ile ikiwakilishwa hapa katika siku za mwisho. Yeye alikuwa na huduma ya aina gani? Mwangalieni Yeye, kama vile nimekuwa nikiwaelezea kote, kuwathibitisha.

²⁴¹ Hebu tumchukue Myahudi mmoja. “Alikuwa kwa walio Wake; walio Wake hawakumpokea.” Watu wa kwanza kabisa waliomjia walikuwa ni Andrea na Filipino. Sijui ni kitu gani kilichoelelea katika mazungumzo hayo, nyumbani pamoja na Yesu usiku huo wakati walipomfuata. Lakini kesho yake, Andrea alikuwa ameridhika kabisa ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi. Yeye alimwonyesha jambo fulani, mpaka akaenda moja kwa moja kwa Petro, ndugu yake, ama—ama Simoni, naye akasema, “Usije sasa twende tukaone kama hii ndiyo.” Akasema, “Tumempata Masihi.”

²⁴² Naweza kuwazia Petro akisema sasa, “Sasa, Andrea, sasa hebu nikwambie jambo fulani, mwanangu. Sasa, unajua baba yetu mzee alikuwa ni Mfarisayo mwema. Naye alitwambia, ninakumbuka nikiketi kando ya mtumbwi siku moja, akaniambia, akasema, ‘Sasa, sasa, sasa, Simoni, baba ametarajia kumwona Masihi. Na hapana shaka ila kabla hajaja Masihi kutakuwako na kila namna ya mambo yatakayotukia, kila namna ya itikadi itainuka. Lakini hebu niwe na hakika. . .’ Na yalikuwako. Loo, naam. Watu walikuja, wakawapoteza maelfu, kisha wakaangamia, na kila kitu. Lakini, yeye alisema, ‘Lakini hebu niwaambie. Hatuna budi kudumu na Neno, Simoni. Sasa, Biblia inasema, Musa, mtumishi wetu, mtumishi wa Mungu kwetu, alitwambia, ya kwamba, “Bwana Mungu wetu angemwinua huyu Masihi, na Yeye angekuwa nabii kama Musa.” Sasa, sasa, Simoni, kama ukimwona katika siku zako. . . Mimi ni mkongwe sana sana. Sitamwona katika siku zangu. Lakini kama—kama ukimwona katika siku zako, kumbuka, Yeye atakuwa ni Mungu-Nabii.” Kwa hiyo Simoni alikuwa na hayo moyoni mwake. Akasema, “Vema, Andrea. Nitapanda niende kwenye mkutano.”

243 Mara tu alipoenda Mbele za Bwana Yesu, Yeye alisema, “Jina lako ni Simoni. Baba yako alikuwa ni Yona.” Hilo lilitosha. Alipewa funguo za Ufalme. Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi.

244 Hapa akaja Myahudi mwingine imara, kasema, “Sasa, ngoja kidogo. Kama Masihi angalikuja, Yeye angalishuka kwenye ushoroba wa Mbinguni, kisha ashuke kwenye hekalu letu kubwa zuri tulilolijenga hapa mahali fulani, kama vile watu wengine hapa wanavyoamini ya kwamba Yeye atakuja kwenye hekalu fulani. Na Yeye atashuka hapa, Naye atatusa papa *hapa*, nao Malaika watakuwa wakiyapigapiga mabawa yao, kila kitu. Wasame, *Huyu* ndiye Masihi. *Huyu* ndiye Masihi. *Huyu* ndiye Masihi.’ Hivyo ndivyo itakavyokuwa.”

245 Ninaweza kumsikia Filipo akisema, “Ngoja kidogo. Ninyi si wa Kimaandiko pamoja na hilo. Dumuni na Neno. Musa alitwambia Masihi angekuwa nini? ‘Bwana Mungu wako atawaondokeshea nabii.’ Mnamkumbuka mzee yule aliyekuwa kule, jina lake Petro, Simoni?”

246 “Naam. Loo, maskini jamaa huyo asiye kuwa na elimu yoyote? Naam. Ninamkumbuka. Naam. Ninamkumbuka.”

247 “U—ulinunua samaki wachache kutoka kwake, naye asingeweza kutia saini risiti yako.”

“Naam. Vema, ninamkumbuka. Ninamkumbuka. Naam.”

“Mbona, wakati alipokwenda hapo juu... Unamjua baba yake?”

248 “Vema, hakika. Bila shaka nilimjua baba yake vizuri sana. Yeye alikuwa ni Mfarisayo halisi, naam, mwanachuoni halisi. Naam.”

249 “Vema, wakati Simoni alipoenda mbele Zake, Yeye alimwambia jina lake lilikuwa ni nani, na jina la baba yake.”

250 “Ah, sasa ninaamini wewe umeingia wazimu. Acha niende, nione. Kamwe hatayasoma mawazo yangu. Nitaenda nikajionee.”

251 Anapanda pale juu, Mbele za Yesu, ndipo Yesu akasema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

Akasema, “Ulimwambia ulikuwa unakuja kunitafuta?”

Kasema, “La.”

252 Akasema, “Rabi,” ambalo linamaanisha *bwana* ama *mwalimu*. “Ni lini Wewe ulipata kuniona mimi? Ndio kwanza nije kwenye mkutano huu usiku wa leo. Ulipata kuniona lini Wewe?”

253 Kasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Ni macho ya jinsi gani!

254 Yeye alisema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli.”

255 Lakini pale walisimama wale ndugu wakubwa mno wa kimadhehebu wamesimama pale. Wakasema, “Mnajua nini? Yeye anafanya hayo kwa Beelizebuli.” Mnaona? Ilibidi walijibu kusanyiko lao. Walikuwa na hati za utambulisho wa duniani.

256 Yeye alikuwa na za Mbinguni, mnaona, maana Musa alisema, “Yeye atakuwa ni nabii,” Naye huyu hapa, akithibitisha kwamba Yeye alikuwa ni Nabii. Hiyo ni kweli. Alithibitishwa. Agizo Lake lilithibitishwa.

257 Kwa hiyo akasema, “Sasa, ninajua ya kwamba Jamaa huyu kweli hufanya hivyo. Lakini Yeye. . .” Ilibidi alijibu kusanyiko lao. Kasema, “Kwa Beelizebuli Yeye hufanya hivi, Yeye huwatoa pepo.”

258 Yesu akageuka, akiyajua mawazo yao. Akasema, “Mkisema hivyo dhidi Yangu, Mwana wa Adamu, nitawasamehe hilo.”

259 Sasa, kamwe hawakusema hivyo kwa sauti. Biblia ilisema, “Waliwazia hilo mioyoni mwao, na Yeye akayajua mawazo yao.” Kuliweka sawa. Naam, bwana. Kasema, “Wao, waliwazia mioyoni mwao.” Mnaona? “Yeye alijua mioyo yao, mawazo yao.”

260 Kasema, “Sasa, mkisema hayo dhidi yangu, Mwana wa Adamu, nitawasamehe. Lakini siku moja, huko chini kabisa katika ulimwengu wa Mataifa, mnaona, Roho Mtakatifu atakuja nikiisha kuondoka, na Yeye atafanya jambo lile lile. Basi kusema neno moja dhidi Yake hakutasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao.”

261 Kabla hajaondoka duniani, Yeye alisema jambo hili. Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu.” Ninataka kutoa tamshi hili, kisha nifunge. “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, huko chini katika Sodoma,” hebu tuone jinsi ilivyokuwa.

262 Yeye alirejea, kwanza, kwenye—kwenye siku za Nuhu. Akasema waliyokuwa wakifanya. “Wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa.”

263 Lakini Yeye alipofika Sodoma, angalieni yale aliyofanya huko Sodoma. Huko Sodoma: Yeye alirejea *hilo* kwa ajili ya wakati *huu*. Sasa, kumbukeni, Wasodoma walikuwa Mataifa. Mnaona? Angalieni. Ndipo kukaja Watu watatu, siku moja, kwa Ibrahimu.

264 Sikuzote kuna matabaka matatu ya watu, hayo ni: wasioamini, wanaojifanya waaminio, na waaminio. Tungali tunao siku hizi. Hiyo ni kweli. Wasioamini, wanaojifanya waaminio, na waaminio; Wasodoma, Walutu, na Waibrahimu.

265 Ibrahimu alikuwa na ahadi. Alikuwa ni kundi lililoteuliwa, likaitwa litoke na lililokuwa limejitenga, kama vile Kanisa halisi la Mungu aliye hai limejitenga na mambo ya ulimwenguni,

maana alikuwa akiitumainia ahadi ya Mungu. Wale Malaika walienda wapi, kwanza? Kwa Ibrahimu.

²⁶⁶ Ilikuwa? Wawili wa hao walishuka kwenda Sodoma, akina Billy Graham mamboleo, huko Sodoma, wakaihubiri Injili, si miujiza mingi, waliwapofusha tu. Kulihubiri Neno huwapofusha. Kwa hiyo hawakufanya miujiza mingi, bali walikuwa wakiita, “Tokeni kwake.”

²⁶⁷ Bali kulikuwa na Mmoja aliyezungumza na Ibrahimu. Mwajua, Ibrahimu alishikwa na hisia ya ajabuajabu. Mwajua, kulikuwa na kitu fulani kuhusu Mtu huyo, ambacho kilikuwa kidogo ni tofauti, na kwa hiyo akamtazama kidogo, mwajua. Naye akamwambia Sara, kasema, “Sasa, wewe rudi hemani.”

²⁶⁸ Hakika, sasa katika siku hizo wakati mgeni alipokuja, wanawake hawakufanya kama wafanyavyo siku hizi. Inawabidi kukimbia mara moja nje na kujianika, na kupachukua mahali pa mume. “Nawe huwezi kuuza hicho, John, isipokuwa nikwambie.” Mnaona?

²⁶⁹ Wanawake walikuwa na uadilifu zaidi katika siku hizo. Walibaki nyumbani, mnaona. Kwa hiyo Wao wakatoka huko nje, naye Sara akabaki hemani.

²⁷⁰ Kwa hiyo akakimbia ndani, kasema, “Sara, kanda unga kidogo upesi sana. Utoe mabonge yote kwake. Oka michache mekoni, mikate michache.”

²⁷¹ Akaenda akachukua ndama, akamchinja. Kisha akaenda, kasema, akawaambia, “Itayarisheni sasa na muiweke tayari.”

²⁷² Akatoka huko nje akatwaa kifukuza nzi, ndipo akaanza kuwawinga nzi. Kisha akaitawadha miguu Yao.

²⁷³ Yeye alijua, kunacho kitu kidogo kinachowaka moyoni mwake. Unaweza tu kujua, wajua, kitu fulani. Akasema, “Hilo hapo agizo, ninaamini. Sasa, jambo pekee, laiti ningeliona tu hilo agizo likithibitishwa. Ninaamini wanalo.”

²⁷⁴ Akasema, “Unajua, Wewe—Wewe ulipitia hapa, kuniona mimi. Hiyo ndiyo sababu ya Wewe kuja huku.” Hiyo ilikuwa sawa. Mnaona? “Ketini chini ya mwaloni, kidogo, mkapumzike.” Kwa hiyo akawatawadha miguu Yao, wakati wakiviandaa vitu hivyo.

Wakaketi wakala.

²⁷⁵ Na—na huyo alikuwa ni Mungu, Mungu Mwenyezi. Biblia ilisema alikuwa. Angalieni huko mwone kama halisemi herufi kubwa B-w-a-n-a, Elohimu. Hiyo ni kweli.

²⁷⁶ Kama vile mtu fulani alivyosema, mara nyingi, kasema, “Huamini huyo alikuwa ni Mungu.”

Nikasema, “Alikuwa Mungu. Biblia ilisema alikuwa.”

“Wewe...” Kasema, “Mungu katika mwili huo, akila nyama?”

277 “Hakika alikuwa. Biblia ilisema hivyo. Hu—hutambui jinsi Yeye alivyo mkuu.” Hiyo ni kweli. Nina furaha Yeye anaweza kufanya hivyo.

278 Vema, jambo pekee, mwajua, tumefanyizwa tu kwa elementi kumi na sita: petroli, nurulimwengu, kalisi, potashi, na vitu vichache namna hiyo. Vema, Yeye aliunyoa tu mkono na kuchukua konzi moja ya hizo, akafanya, “Whiu! Ingia ndani, Gabrieli,” mnaona, yule Malaika. Akachukua konzi nyingine, akafanya, “Whiu!” Kasema, “Ingia ndani, Mikaeli.” Akafanya, “Whiu!” akaingia ndani yake, Mwenyewe. Nina furaha sana kwa hilo. Mnaona? Akaja akitembea, kasema, “Ninashuka chini.” Huyu ni Mungu wetu.

279 Moja ya siku hizi, elementi hizi zote zitaondoka. Lakini Yeye atasema, “William Branham?”

Nitasema, “Mimi hapa, Bwana.” Yeye ni mkuu. Naam.

280 Kasema, “Sina budi kujiwakilisha Mwenyewe mbele ya mtumishi Wangu huko chini, nami ninataka kuwa mtu kama yeye.” Kwa hiyo alishuka tu chini, akaketi pale chini, mavumbi nguoni Mwake, akaketi chini akala. Akaketi chini.

281 Akakaza kuangalia kuelekea Sodoma, mwajua. Ibrahimu alijua kulikuwa na kitu fulani kinachoendelea, maana hapo ni maskini mahali paovu sana, mwajua. Kwa hiyo akaendelea kuwazia juu yake, namna hiyo. Akasema . . .

282 Sasa, kumbukeni, jina lake lilikuwa Abram, nalo jina la Sara lilikuwa S-a-r-a, Sara. Na siku chache kabla ya hapo, Mungu alikuwa amekutana naye katika ono na kulibadilisha jina lake likawa Ibrahimu, nalo jina la mke likawa Sarah, S-a-r-a-h. *Sarah*, “binti mfalme.” *Ibrahimu*, “baba wa mataifa.”

Kwa hiyo Yeye alisema, “Ibrahimu.”

283 Ibrahimu akasema, “Loo—loo. Najua nilisema kweli. Kuna jambo fulani kuhusu Mtu huyu lililo tofauti.”

284 “Ibrahimu, yu wapi mkeo,” S-a-r-a-h, “Sarah? Yu wapi Sarah, mkeo?”

Yeye alijua papo hapo. “Loo,” akasema, “yuko hemani.”

Nayo Biblia ilisema, “Ilikuwa nyuma Yake. Hiyo hema, nyuma Yake.”

285 Akasema, “Ibrahimu, Mimi . . .” Kiwakilishi nafsi; Yeye yule aliyezungumza naye. “Nitakuzuru kulingana na majira ya uhai, unaona, pamoja na Sara, nawe utampata mtoto huyu mchanga ambaye umekuwa ukimngojea. Wewe una umri wa miaka mia moja sasa, naye tisini. Lakini, Mimi, nitakupatia mtoto huyu mchanga niliyekuahidi, maana umekuwa mwaminifu, kungojea.”

286 Naye Sara, huko nyuma kwenye hema, akasema, “Uhu.” Kamwe hakulisema kwa sauti. Akacheka, kimoyomoyo, kasema,

“Ati mimi, mwanamke mkongwe, nipate raha tena, na bwana wangu, mzee namna hiyo?” Kasema, “Isingewezekana kabisa. Jamaa huyo, kwani Yeye anazungumza kuhusu nini?”

Malaika akasema, “Kwa nini Sara akacheke?” Hum!

²⁸⁷ Ilikuwa ni kitu gani? Akaelekea Sodoma. Mara baada ya kuzuriwa na Malaika huyo, ishara hiyo ya mwisho iliyotolewa, ishara ya mwisho iliyotolewa, Sodoma ikateketezwa kwa moto.

²⁸⁸ Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

²⁸⁹ Mungu amelishughulikia Kanisa Lake, kotekote, kwa ishara, maajabu. Lakini jambo la mwisho lilikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili wa Kanisa Lake, kama vile alivyokuwa katika mwili wa mwanadamu kule, na kuonyesha ishara hiyo hiyo, ya kwamba Masihi tayari alikuwa amejikwakilisha Mwenyewe miongoni mwa watu, kabla tu moto haujashuka katika siku za mwisho: hati ya utambulisho, kuthibitisha ya kwamba Neno ambalo Yesu aliahidi ni Kweli. Na tuombe.

²⁹⁰ Baba yetu wa Mbinguni, ni Neno Lako, thibitisho la agizo. Hilo ni Neno Lako, Baba. Tunaweza tu kulizungumza. Ninaomba kwamba ulithibitishe, Bwana. Nami ninajua ya kwamba...Nasa-...naomba kwamba Wewe utanisamehe wasiwasi wangu, na—na ujinga wangu, yote kuhusu hilo, na uliondoe hilo niani mwa watu, njia yangu mbaya, iliyokatikakatika ya kujaribu kuuleta ujumbe. Na—naye Roho Mtakatifu akinigusa, si—si—sijui jinsi ya kufanya ila kuutoa tu, Baba, nikiketi hapa pamoja na wanaume na wanawake ambao ni wasafiri na wageni.

²⁹¹ Wakati, ulimwengu mzima unatikisika, siku hizi. Wao—wao wanasema sasa, katika siku chache, sasa watamrusha mwanadamu kuizunguka dunia, katika mzingo, wamzungushe duniani, wakijaribu kumpeleka mwanadamu mwezini. Ulimwengu mzima, unatetemeka na kutikisika. Mataifa madogo, kila mahali, pamoja na makombora yatakayochimba shimo ardhini, kina cha futi mia moja na hamsini, kwa maili mia mbili na hamsini ama mia tatu mraba. Matatu ya hayo wakati mmoja yangeizamisha dunia nzima. Ulimwengu wote uko katika hali ya jakamoyo.

²⁹² Makanisa yameliacha Neno. Kuna kila namna ya mashirika na madhehebu yanayobeba hati za utambulisho za kilimwengu. Na—na kama wewe si mfuasi wao, huwezi kukichomoza kichwa chako katika moja ya makanisa yao.

²⁹³ Lakini, hata hivyo, kama ilivyokuwa huko nyuma katika wakati wa Nuhu, kama ilivyokuwa kote katika Biblia, Wewe bado utawatuma manabii wako na watumishi, Bwana, pamoja na agizo, pamoja na thibitisho nyuma yake. Mungu, nina furaha sana kwa hilo, kwamba Wewe uliliahidi.

294 Na sasa, Bwana, Wewe ulisema, “Msiogope, enyi Kundi dogo. Kundi dogo, ni mapenzi ya Baba yenu kuwapa Ufalme.”

295 Ulisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, wakati lile kundi dogo lilipookolewa tu kwa maji, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Siku za Lutu, wakati... Katika wakati wa Nuhu, “Walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa.” Basi liangalie siku hizi, Baba, tunalionga hilo. Sasa, huo ulikuwa ni kwa ulimwengu wenye dhambi uliokuwa ukifanya hivyo.

296 Basi sasa angalia siku za Lutu, jinsi upotovu, walawiti! Loo, jinsi ambavyo ulimwengu, nchi nzima, karibu serikali yetu yote imemezwa nao, na kila mahali. Loo, tumeliwa na wadudu, Bwana, na pepo na nguvu za adui.

297 Ulimwengu mzima umetishwa kabisa. Na ninii yetu yote...Hata taifa letu ni kama mvulana mdogo anayepitia makaburini usiku, akipiga mbinja, kujizuia asiogope. Tunajua yako mlangoni.

298 Kanisa, Bwana, Wewe ulisema, “Inueni magoti yenu... Inueni macho yenu vitu hivi vitakapoanza kutukia. Ukombozi wenu unakaribia.”

299 Roho Mtakatifu amemwagwa juu ya Kanisa Lako. Wewe umewaita watu wa kila taifa, Mmeksiko, mzungu, Mwanglo-Sakson, mweusi, Mhabeshi, jamii zote mbalimbali, kote ulimwenguni. Kama vile maskini wamishenari Wako waliojazwa na Roho Mtakatifu wa kale walivyoenda, wenye njaa, wakifa kwa njaa, wengi wao wakauawa, wakasulubiwa, wakafanyiwa mizaha, na kila kitu kingine. Wameenda bila ya kanisa lolote kubwa kuwadhamini. Walienda kwa agizo la Mungu, pamoja na, “Ishara hizi zikifuatana na hao waaminio.” Nimekutana nao kwenye huduma za kimishenari huko ng’ambo, Bwana. Tumekuwa na nguvu kuu za Mungu, kunena kwa lugha, kufasiri lugha. Tumekuwa na mabatizo ya Roho Mtakatifu, madhihirisho ya nguvu.

300 Na sasa, Bwana, kama vile ulivyomchukua Ibrahimu, akiwawakilisha walio Wateule, walioitwa watoke. Ulimleta Ibrahimu kupitia hilo jangwa, ukamtenganisha. Ulimwonyesha kila namna ya ishara. Lakini ishara ya mwisho ilikuwa ni wakati Mungu, Mwenyewe, alipojidhihirisha Mwenyewe katika mwili.

301 Yesu, Wewe ulisema, “Kama ilivyokuwa katika siku hiyo, ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana wa Adamu.” Njoo, Bwana. Hili ni Neno Lako, vizuri nilijuavyo. Ninaliamini Hilo, Bwana. Kunao wengine hapa wanaoliamini. Jalia litukie tena, Bwana. Jalia litukie katika Tempe, kama thibitisho la kukaribia kwa Bwana Yesu. Tujalie, Bwana. Lingetutia nguvu sisi sote, Bwana. Lingewatia nguvu ndugu hawa. Lingewatia nguvu wahudumu Wako kila mahali. Lingewatia nguvu walei. Lingetufurahisha sisi sote. Tujalie, Baba.

³⁰² Sasa, umbali ninaoweza kwenda ni kulihubiri Neno Lako. Sasa, Bwana, inakuhitaji Wewe kufanya thibitisho hilo. Siwezi. Lakini kama ni agizo, nimehubiri Ukweli, ninaamini, Baba wa Mbinguni, kwamba Wewe utaithibitisha kwa ishara na maajabu ambayo uliahidi yangekuwa katika siku hizi. Tujalie, sasa. Ninajikabidhi Kwako, pamoja na kanisa hili, pamoja na Neno. Sasa, Baba, tutakungojea Wewe, kama utatuonyesha tu ya kwamba Wewe uko miongoni mwetu. “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Hiyo ni ahadi Yako.

³⁰³ Tena, Baba, jinsi ambavyo lingewaimarisha baadhi ya ndugu zangu hapa, jinsi lingeliimarisha kanisa; hicho kitu ambacho si cha kubuni tu, kitu fulani ulichosema, “Naam, nimesikia haya yakihubiriwa wakati wote.” Lakini, Baba, jalia waone kwamba Wewe ni Mungu unayelitimiza Neno Lako. Sasa, itahitaji zaidi ya mimi, Baba. Itahitaji kanisa hili lote katika moyo mmoja. Itahitaji imani halisi kufanya hivyo. Lakini ninaomba, Baba, ya kwamba utalijalia kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu. Amina.

³⁰⁴ Sasa, enyi marafiki, mstari wa maombi. Loo, samahani. [Ndugu O'Donnell anasema, “Endelea moja kwa moja. Ni sawa.”—Mh.]

³⁰⁵ Samahani kwa tabia zangu zinazosisimua, zilizokatikakatika mimbarani. Na—naomba mtanisamehe. Lakini ndio kwanza nimalize kusoma Baraza lililotangulia Nikea. Pia nimekichukua *Babeli Mbili* cha Hislop, na *Kanisa Linalosafiri* cha Broadbent, Baraza lililotangulia Nikea, Baraza la Nikea, na Baraza lililofuata lile la Nikea, *Wazee wa Nikea*, kuona jinsi Roho Mtakatifu alivyowaongoza. Hata hawakuwa na madhabahu kanisani mwao. Hawakuwa na kitu kama msalaba wenye sanamu. Katoliki ya Kirumi liliendelea na fundisho la sharti, pamoja na msalaba wenye sanamu. Lakini waorthodoksi halisi walikaa mbali nalo, walikuwa na majengo madogo yasiyo na kitu ila mabamba tu. Nao wangeninii. . . Mtu fulani mtauwa angelielezea Neno la Mungu, nazo nguvu za Mungu zingeshuka. Wangeinua tu mikono yao na kumsifu Mungu. Wengenena kwa lugha, na ishara na maajabu zingewafuata. Naam, bwana.

³⁰⁶ Polikapu, Ignasio, Martin, Ireneo, Columba, loo, jamani, Justin, ni wangapi zaidi wa watauwa halisi ambao wasingevumiliana na hilo kanisa lingine hata kidogo, upande wake wa Kirumi. Walidumu katoliki. Sisi ni katoliki, pia, katoliki ya kimitume. Sasa, *katoliki* linamaanisha “la ulimwenguni kote.”

³⁰⁷ Lakini Katoliki ya Kirumi ilichukua msalaba wenye sanamu na mafundisho ya sharti, na kadhalika namna hiyo, na kusema, “Sio Biblia.” Wao, “Mungu alikuwa katika kanisa Lake.”

³⁰⁸ Mungu yuko katika Neno Lake. Biblia ilisema, “Kama mtu yeyote ataondoa ama kuongeza chochote Kwake, huyo

ataondolewa, sehemu yake, kutoka kwenye Kitabu cha uzima.” Tunaamini tu yale Mungu aliyosema, na ni hivyo tu. Sasa, kwa hiyo, tungali tunaamini Ujumbe huo.

³⁰⁹ Sasa, kuna watu wagonjwa hapa usiku wa leo. Nimewahubiria, kwamba Mungu hulithibitisha agizo Lake. Hiyo ni kweli. Mungu huliangalia Neno Lake, kulithibitisha. Jambo pekee analojaribu kufanya ni kupata moyo ambao Yeye anaweza kuingia.

³¹⁰ Sasa, usifikiri kwamba utafanya hilo kupita kiasi. Hutalifanya. Ungeweza kuwazia sa—samaki mdogo yapata urefu wa nusu inchi, huko katikati ya bahari huko ng’ambo, akisema, “Afadhali ninywe maji haya kwa unyimifu. Huenda nikaishiwa”? La hasha. Vema, kamwe usingeweza kuzimaliza nguvu za Mungu na wema wa Mungu. Hakika usingeweza, kwa hiyo fungua tu.

³¹¹ Unasema, “Vema, nilimpokea Roho Mtakatifu.” Loo, kuna ninii—ninii tu. . .

³¹² Mbingu zote zimejaa Huyo. Mnaona? Mungu anajaribu tu. . . kama vile. . . Kama zingalikuwa ni zote, mbingu zote, zingalikuwa bomba kubwa mno unaosimama wima, nawe ulikuwa na ufa mmoja mdogo. Yeye anajaribu kulundika. . . Hayo maji yatajaribu kujisukumiza yatoke. Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu anavyojaribu kujisukumiza Mwenyewe ndani yako, namna hiyo, namna hiyo, akijaribu kukufanya uliamini Hilo. Ninajua hiyo ni Kweli. Sasa, ninaamini kwamba. . . Wao walitoa. . .

³¹³ Hivi alisambaza kadi za maombi, nitaomba? Ninaamini alizisambaza. [Ndugu wanasema, “Naam.”—Mh.] Vema. Vipi. . . Yuko wapi? Ati nini? Samahani. Moja hadi hamsini. Vema. Hatuwezi kuwasimamisha wote wakati mmoja. Kwa hiyo hebu tuwasimamisha labda. . . Mbona, hilo ni sawa, simameni tu kimya. Mnaposongea, labda safu hii ndogo hapa irudi nyuma, wapate kusonga kidogo. Kuna bilauri ya maji, ninaamini, iliyowekwa pale, kama mtaiangalia. Vema.

³¹⁴ Hebu tuchukue namba moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi. Hebu wasimame. Namba moja, ni nani aliye nayo? Kadi ya maombi namba moja? Ni kadi tu ya maombi iliyo na namba juu yake. Namba moja, mbili, tatu, nne, namna hiyo. Namba moja, kadi ya maombi, ni nani aliye nayo? Hakika kuna kasoro fulani.

³¹⁵ Semeni katika Kihispaniola. Namba *moja* ni nini, katika Kihispaniola? [Mtu fulani anasema, “Uno.”—Mh.] Uno. Uno, ni nani aliye nayo?

³¹⁶ Namba moja? Wasemaje? Vema, papa hapa. Namba mbili, ni nani aliye nayo? Namba tatu, nne, tano, sita, saba, nane? Moja, mbili, tatu, simameni tu papa *hapa*. Tutafanya mstari. Huh? Naam. Ni sawa. Vema. Hilo ni sawa. Vema. Moja, mbili, tatu, nne,

tano, sita, saba, nane, tisa, kumi. Hebu waje. Zungukeni kabisa mje upande *huu*, mkiweza.

317 Iwapo huwezi kuamka sasa, inua mkono wako. Tutahakikisha kwamba utafika hapa. Tutaona. Mtu fulani atakuleta hapa. Mnaona?

318 Sita, saba, nane, tisa, kumi. Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini. Acheni waje, kuanzia moja hadi ishirini sasa, pangeni mstari *hapa*. Vema. Hiyo ni kweli.

319 Sasa, ikiwa mna kadi zenu, njoni huku, marafiki. Usi—usi—usibaki nyuma, maana unamnyima mtu mwingine nafasi, mnaona. Usiogope kuja, iwapo ulichukua kadi yako. Njoo, kama walikupa kadi.

320 Sasa, huyu mvulana huja na hizi kadi, kwanza. Anasimama hapa juu na kuzichanganya, pamoja, hamsini ama mia moja, ama chochote afanyacho. Anashuka moja kwa moja mstarini, anampa mtu yeyote. Mtu mmoja huenda akapata “moja,” huyo mwingine “kumi,” huyo mwingine “hamsini,” na huyo mwingine “tisini,” namna hiyo. Hatujui walipo. Wametawanyika kote. Hilo linamwacha huyo mvulana ambapo hajui nini. Halafu, huyo mvulana hajui nitakapoanza kuitia, usiku huo. Maana, mnaona, sijui, mimi mwenyewe. Huenda nikaanzia. . . Ni wangapi wamekuwa mikutanoni hapo kabla, nao wanajua mimi huruka kote kupitia kwake? Hilo ni sawa. Mnaona?

321 Kwa hiyo, mara nyingi, watu wanaogopa kuja huku, kwa maana dhambi zao zinatajwa hapa. Sasa, kama umefanya kosa lolote, na hutaki litajwe, afadhali usije, hivyo tu, maana Yeye hakika atafanya hivyo. Aa-ha. Ni wangapi wanaojua jambo hilo ni kweli? Naam, bwana. Bila shaka ni kweli. Sasa, iwapo wewe—iwapo wewe umehukumiwa na uko chini ya dhambi, mbona, usije. Lakini kama huhukumiwi, kama uko chini ya Damu, njoo. Mnaona? Vema.

322 Sasa, sawa, vema, tutaanza tu papa hapa tuone tunapoweza kwenda.

323 Sasa, ni wangapi humu ndani walio wagonjwa, nao waliingia wala hawakupata kadi ya maombi, mlichelewa kupita kiasi ama kitu fulani? Inueni mikono yenu, kila mahali, kote jengoni, vema, huna kadi ya maombi.

324 Sasa, palikuwapo na maskini mwanamke mmoja aliyepitia kwenye umati. Labda hakuwa na kadi ya maombi, bali aligusa upindo wa vazi Lake. Hilo lilitosha. Vema. Akaugusa upindo wa vazi Lake, naye akaponywa.

325 Sasa, ninyi huko nje mnaoamini kwa moyo wenu wote, ninyi ambao kweli mnaliamini hili kwa moyo wenu wote, semeni tu, “Bwana Yesu, ninaamini hili kwa moyo wangu wote,

nami nitakukubali Wewe, na kuamini ya kwamba...Ninajua ya kwamba Ndugu Branham hanifahamu, ama kujua lolote kunihusu mimi. Laiti ungaliniruhusu tu niguse vazi Lako!" Sasa, Biblia inasema...

³²⁶ Sasa, wahudumu watashuhudia hili. Biblia inasema, kwamba, "Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Hiyo ni kweli? "Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Ndivyo alivyo, sasa hivi.

³²⁷ Vema, basi, ikiwa Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, Kuhani Mkuu huyo angefanyaje wakati akiguswa? Iwapo Yeye ni Yesu yeye yule aliyekuwa huko nyuma, Yeye angetenda vile vile. Hawezi kubadilisha njia Zake. Hawezi.

³²⁸ Kama Yeye alisema huko nyuma, "Vema, niliwaokoa kwa sababu waliniamini Mimi, bali leo hii ni—ni—nitawaokoa kwa kuwa wana fedha nyingi sana," Yeye hawezi kufanya hivyo.

³²⁹ Hana budi kubaki na msimamo Wake wa kwanza. Mnaona? Mungu anapofanya uamuzi, ni mkamilifu. Hauwezi kubadilishwa kamwe, hata kidogo. Mungu kamwe habadilishi mpango Wake, mnaona, kwa hiyo kama Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, nawe ulingusa kwa imani yako...

³³⁰ Sasa, Yeye hana mikono yoyote duniani ila yangu na yako. Hiyo ni kweli? "Mimi ndimi Mzabibu; ninyi ni matawi." Sasa, Mzabibu hauzai tunda, sivyo? Matawi ndiyo yanayozaa tunda. Kwa hiyo Mzabibu hulihuisha tu hilo tawi, bali wewe unalionga tawi. Mzabibu haujafanyizwa kufanya hivyo; mnaona, Yeye yuko Utukufuni. Yeye ni Roho Mtakatifu. Sasa, Yeye hazai tunda, bali Yeye hukutia nguvu wewe na mimi, ili tupate kufahamiana sisi kwa sisi, kupitia kwa sauti, ambazo Yeye hunenea kupitia kwetu na kufanya kazi Zake, apate kulithibitisha lile agizo ambalo tumetumwa kutekeleza. Mnalielewa sasa, kila mtu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

³³¹ Sasa ninyi ombeni, nawe unasema, "Bwana Yesu, nitaliamini hili kwa—kwa moyo wangu wote. Ni—ni—nitajaribu kuliamini kweli kwa yote yaliyo ndani yangu. Nami ninaamini ya kwamba Wewe uta—utanifanya mzima. Nami ninaenda, kwa moyo wangu wote, kujaribu kuugusa upindo wa vazi Lako, nikiamini ya kwamba Wewe utanipa afya." Sasa, wewe amini tu hilo, ama mpendwa wako.

³³² Sasa, nitawaulizeni. Pamoja na yale...Sasa, mnajua mimi ni mpentekoste. Ni—ninaamini katika kupaza sauti, kumsifu Bwana. Bali nitawaombeni kufanya jambo hili. Sasa, tunapokuja, ninawatakeni mwe na kicho sana mwezavyo. Sasa, jifiche tu sasa. Weka mbali mashaka yako yote, na kusema

tu, “Sasa, Bwana, nisaidie.” Mungu atafanya hilo, iwapo tu utaliadini.

333 Sasa, sasa, huyu hapa mwanamke amesimama. Sijawahi kumwona maishani mwangu.

334 Sasa, yeyote yule aliye kwenye *huu* hapa. Wakati mwingine sijui yale ninayosema; kama ikinigusa, ni ono. Kama ikiwa nyinyi. . . Mnaweza kunisikia vizuri sasa? Vema. Sasa iweni tu na kicho kabisa.

335 Sasa, huyu hapa mwanamke amesimama. Sasa, hii hapa picha nzuri ya Biblia. Sisi hatufahamiani. Sikujui wewe. Sasa, huenda ukanifahamu, kwa kujua mimi ni Ndugu Branham. Lakini mimi sikujui, kwa vyovyote vile.

336 Sasa, hii ni picha kama ilivyokuwa katika Yohana Mtakatifu 4. Yesu alikutana na mwanamke ambaye kamwe hakuwa amemwona, ama kamwe hakumjua. Alijua kwamba Yeye alikuwa ni Myahudi, bali hayo ndiyo yote aliyojua. Ndipo Yesu akazungumza na mwanamke huyu kidogo. Alikuwa akifanya nini? Alikuwa akiwasiliana na roho yake. Mnaona?

337 “Alihitaji kupitia Samaria. Basi alipokuwa akipitia Samaria. Alikutana na mwanamke huyu.” Kwa nini? Baba alimwongoza hata Samaria. “Panda uende Samaria.”

338 Yeye hakujua la kufanya. Mwanamke huyu akatokea. Akawazia, “Labda hili ndilo Baba analotaka.” Kwa sababu, Yeye alisema. . .

339 Akiisha kumponya yule mtu kwenye. . . aliyekuwa ni kiwete, si kiwete, bali nadhani huenda alikuwa na ugonjwa uliodumaa. Katika Yohana Mtakatifu 5, mlango unaofuata, naamini ndivyo. Alipitia karibu na birika la Bethesda, na hapo alilala mtu aliyekuwa amedhoofika kwa miaka kadhaa, alikuwa hawezi. Sasa, angeweza kutembea. Lakini Malaika alishuka na kulitibua lile birika. Ninyi ndugu mnajua mahali ninapozungumzia. Ndipo Yesu akapitia pale, na kusema, akasema, kuhusu kwenda kwenye hilo birika, akasema, “Sina mtu wa kunisaidia. Mtu fulani anaweza kufanya vema kuliko mimi. Anaweza kunitangulia kwenda birikani,” kwa maneno mengine.

340 Akasema, “Jitwike kitanda chako uende nyumbani mwako.” Akajitwika kitanda chake akaenda zake.

341 Sasa, Yesu kamwe hakumponya mwingine wao, na kulikuwako na umati, maelfu. Kwa nini hakufanya hivyo? Hilo hapo moja kwa ajili ya kusanyiko, kwa ajili ya sisi wahudumu. Mungu aliyejaa huruma. Hiyo ni kweli? Umati wa viwete, vipofu, walemavu, waliopooza, kila namna ya watu? Hivi Biblia ilisema hivyo, ndugu zangu? Naye akaenda moja kwa moja kwa mtu mmoja aliyekuwa hawezi. Hakuwa kipofu. Angeweza kutembea. Huenda alikuwa na ugonjwa wa tezi dume. Huenda alikuwa na TB iliyodumaa. Haukuwa unaenda kumwua. Alishakuwa nao

kwa muda wa miaka ishirini na minane, wala haungemuua. Ndipo Yeye akamwendea mtu huyo. Kwa nini? Basi, akamponya huyo tu, kisha akaondoka.

³⁴² Vipi kama angekuja Tempe usiku wa leo na kufanya hivyo? Wangemkosoa papo hapo. Hiyo ni kweli, ndugu zangu? Wangemkosoa. Bali, kumbukeni, Yesu alimjua mtu huyo na alijua kwamba amekuwa katika hali hiyo kwa muda huu wote. Hivyo ndivyo Yeye alivyosema?

³⁴³ Sasa, wakati Wayahudi walipompata mtu huyu, yeye aliwaambia ni Nani aliyefanya hivyo. Walimpata Yesu nao wakampa swali. Mnafikiri wangempa swali usiku wa leo? Hakika.

³⁴⁴ Yeye alisema nini? “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda: hilo atenda Mwana vile vile.” Hiyo ni kweli? Basi, kulingana na Neno Lake mwenyewe, Yeye hakufanya lolote mpaka Mungu alipomwonyesha katika ono jambo la kufanya.

³⁴⁵ Mnamkumbuka Eliya, katika mahubiri yetu usiku wa leo? “Nimefanya haya yote kwa amri Yako.” Nabii yeyote wa Bwana huenda tu jinsi Bwana anavyomwongoza.

³⁴⁶ Sasa hebu tulilinganishe. Sasa, Kristo ni Roho Mtakatifu aliye humu ndani sasa. Sasa, ninaamini ya kwamba nilijisikia kuongozwa kuja Arizona. Yesu alijisikia kuongozwa, alihitaji kupitia Samaria. Nilijisikia kuongozwa kufanya ibada ya uponyaji huku Tempe usiku wa leo, kamwe sijawahi kufanya moja hapa. Sijui ni kwa nini.

³⁴⁷ Vema, imetokea kwamba wewe ndiye mtu wa kwanza hapa juu. Haya basi, Yohana Mtakatifu 4, vivyo hivyo tena. Sikujui. Hunijui mimi. Sijui hata jambo moja. Huenda wewe ukawa ni mwenye dhambi. Huenda ukawa ni mnafiki. Huenda ukawa katika uzinzi. Huenda ukawa ni mtakatifu mtauwa. Huenda ukawa ni mgonjwa. Huenda umesimama kwa ajili ya mtu mwingine. Huenda ukawa na matatizo ya kifedha. Sijui ulilo nalo. Sijui neno kukuhusu. Sasa, hiyo ni kweli, sijui. Sasa, kama hatufahamiani, ili kwamba asiyeamini fulani huenda ameketi hapo karibu, inua mkono wako, kama hatufahamiani, kama hiyo—hiyo ni kweli. Mnaona? Sasa, kama Roho Mtakatifu... katika kuwasiliana na roho yake.

³⁴⁸ Sasa, sote wawili tumesimama hapa, mwanamume na mwanamke, kama tu vile walivyokuwa. Naye Yesu akazungumza naye mpaka akaipata shida yake. Hiyo ni kweli? Sasa, wote wanaojua hiyo ni kweli, semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Alipata shida yake ilikuwa ni gani, na Yeye akamwambia shida yake ilikuwa ni gani.

³⁴⁹ Naye akasema, “Bwana, hapana shaka Wewe ni nabii.” Mnaona, hawakuwa na manabii wowote kwa muda wa miaka mia nne. Akasema, “Hapana shaka Wewe ni nabii. Sasa, tunajua

ya kwamba Masihi ajapo, hii itakuwa ndiyo ishara ya Masihi. Yeye atatwambia mambo yote.” Hiyo ni kweli?

Vema, Yesu akasema, “Mimi ninayenena Ndiye.”

³⁵⁰ Sasa, kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi wakati huo, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele; ila tu, katika umbo la Roho Mtakatifu, akiutumia mwili wangu, roho yangu ninapoisalimisha Kwake, na angeniambia mahali shida yako ilipo, ungejua kama ilikuwa ni kweli ama si kweli, maana wewe ni shahidi wa hilo. Sasa, kama wewe. . .

³⁵¹ Kama nilikuwa na ibada ya uponyaji, nije huku, kasema, “Utukufu kwa Mungu! U mgonjwa, dada?”

“Naam. Ninayo TB”

³⁵² “Utukufu kwa Mungu!” Nikaweka mikono juu yako. “Haleluya! Pokea uponyaji wako.”

³⁵³ Sasa, ndugu wengi wazuri, kama vile Ndugu Oral Roberts na hao wengine, hao ni watu halisi wa Mungu. Hiyo ndiyo karama yao. Wanasema, “Utukufu kwa Mungu! Ninaliamini. Nawe je?”

“Naam.”

³⁵⁴ Ninaamini ungepata afya. Hakika, ninaamini hilo. Naam, bwana. Ninaamini. Ungemwendea mchungaji wako, kama wewe ni Mkristo, ama chochote namna hiyo, ninaamini ungefanya hivyo, ingefanikiwa.

³⁵⁵ Lakini sasa vipi kama Yeye akija na kukwambia jambo fulani ambalo umefanya. Sasa, ungejua kama hiyo ni kweli ama si kweli. Na ikiwa Yeye anaweza kukwambia yale yamefanywa, hakika ungeweza kuamini ikiwa Yeye angekwambia yale yatakayofanywa. Hiyo ni kweli? [Dada huyo anasema, “Kweli.” — Mh.]

³⁵⁶ Sasa, ni wangapi wanaoamini huyo angekuwa ni shahidi, kama Yeye akilifanya, ya kwamba Yeye ni Yesu Kristo aliye Masihi, yeye yule jana, leo, na hata milele? Sasa, kumbukeni, sio mimi. La. Mimi ni kama maikrofoni hii, bubu kabisa. Ningejua? Tayari nimekiri kwenu, na kwake, na sote wawili mmoja kwa mwingine, hatuninii, kamwe hatujawahi kuonana. Kwa hiyo itahitaji nguvu kutoka mahali fulani.

³⁵⁷ Sasa, mnaweza kuamini kama baadhi yao walivyofanya, na kusema, “Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli.” Ama, ungeweza kusema, “Hum. Yeye ni ibilisi, mpiga ramli, namna fulani ya roho mbaya.” Basi, hiyo ni kati yako na Mungu. Mnaona? Sasa, sasa, hiyo ni juu yako, kuamua Hilo. Mnaona? Inategemea tu mtazamo wako Kwake.

³⁵⁸ Lakini, kwangu mimi, ni Yesu Kristo. Ni, kwangu mimi, kwa kuwa ni ahadi Yake. Na sasa kama Yeye alifanya ahadi na kuniagiza mimi, na kunipa ishara hizo. . .

359 Na miaka mingi iliyopita, nilikuwa hapa pamoja nanyi watu, na Yeye akanipa ishara, kama ungeweka mkono wako juu ya wangu. Ni wangapi wanaokumbuka hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ndipo ningeweza kuwaambia, kama ningetulia kwa dakika chache. Nisingekuwa na udhibiti, bali kusema una ki—kivimbe ama chochote kilicho. Ilikuwa ni kamilifu. Hiyo ni kweli?

360 Nami niliwaambia, ya kwamba Yeye aliniambia, “Kama ningekuwa na kicho na kuamini, nami nikae huru,” na, hiyo ni kusema, pasipo kuombaomba pesa. Nami kamwe sijawahi kuchukua matoleo maishani mwangu. Mnaona? Na kila kitu, “Na kuishi mkweli Kwake, ya kwamba ingekuwa, kwamba, ambapo ningewaambia watu siri za moyo wao hasa, jambo lingine.” Hawawezi kukana hilo. Mnaona? Mnaona? Mnakumbuka nikitabiri hayo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa limetimia. Mnaona?

361 Sasa, sasa iweni tu na kicho. Mnasema, “Unangojea nini, Ndugu Branham?” Yeye. Simjui mwanamke huyo. Asiponitia mafuta Yeye, siwezi kulifanya. Ni hayo tu.

362 Ni wangapi wamewahi kuiona ile picha ya yule Malaika wa Bwana, ule Moto, Nguzo yenye moto? Wameipiga picha, wanayo kote ulimwenguni sasa. Iko Washington, DC, katika ukumbi wa sanaa za kidini. Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kuthibitishwa kisayansi.

Nitazungumza tu na wewe kwa dakika moja, kuwasiliana.

363 Naam. Bwana asifiwe. Aa-ha. Huyu hapa. Aa-ha. Siwezi kukwambia jinsi ninavyojua hilo, bali najua Yeye yuko papa hapa sasa. Unaona? Hiyo ni kweli. Yuko papa hapa sasa hivi. Shukrani kwa Bwana. Mnaona? Hii hapa sasa.

364 Una ugonjwa wa ngozi unaotaka niuombee. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa, unaamini hilo kwa moyo wako wote?

365 Sasa, huenda mkasema nilibahatisha hilo. Mnaona? Sasa angalieni muone kama tulilibahatisha. Mnaona? Iweni na kicho sana. Anaonekana kuwa ni mtu mzuri.

366 Sasa, sasa hivi singeweza kukwambia yale niliyokwambia, kwanza. Sasa, hebu kidogo. Naam, ni ugonjwa wa ngozi, ulio nao. Umekuwa nao kwa muda. Hata umeombewa, kwa ajili yake. Halafu, una tatizo fulani ubavuni mwako. Hiyo ni kweli. Lilisababishwa na ajali ya motokaa. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Sasa unaamini, sivyo? Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, ninaomba uponyaji wake. Amina. Nenda, ukiamini.

367 Mnaamini kwamba ni Yeye yule jana, Nuru za jioni za Roho Mtakatifu?

368 U hali gani? Mimi na wewe hatufahamiani, mara ya kwanza sisi kukutana. Kama ningeweza kukuponya, ningekuponya.

Ninamwakilisha tu Mponyaji, kama balozi aliyeagizwa, nikiombea thibitisho Lake. Lakini kama Mungu ataniambia sababu ya wewe kuwa hapa, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama mtumishi Wake? Utaamini?

³⁶⁹ Jambo moja, ni kivuli kimekuzunguka, inaonyesha ya kwamba unaugua ugonjwa wa wasiwasi, kuvurugikiwa na akili, ugonjwa wa wasiwasi. Unakuwa mbaya zaidi wakati wa jioni jua linapoanza kutua. Hiyo ni kweli. Halafu, jambo lingine, una kivimbe kinachokutia hofu. Unaamini Mungu anaweza kuniambia mahali kivimbe hicho kilipo? Kiko kwenye titi la kulia. Hiyo ni kweli? Unaamini sasa? Sasa, kuna Kitu fulani juu yangu, kinachosema hayo, kinachojua hayo. Hiyo ni kweli? Unaamini kwamba ni Mungu? Basi Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Mungu awabariki. Amina.

Iweni na imani. Msitie shaka. Aminini tu kwa yote yaliyo ndani yenu.

³⁷⁰ Maskini jamaa yule pale aliyevaa hiyo tai ya milia, acha tu kuwa na hofu. Yabisi kavu hiyo itakuacha, kama ukiamini tu kwa moyo wako wote. Unaona? Ulikuwa umeketi hapo, ukingojea hilo, sivyo? Wala huna kadi ya maombi. Huihitaji. Amini tu hilo.

³⁷¹ Mnaona, imani yake iligusa Kitu fulani. Mnajua mtu huyo hakunigusa mimi. Yuko futi ishirini kutoka kwangu. Hiyo ni kweli? Lakini aligusa nini? Yule Kuhani Mkuu.

³⁷² Niliangalia hapa penye mwanamke *huyu*, palikuwapo na mwanamume. Nikaangalia, ilikuwa ni mwanauume. Nikasema, “Haiwezekani. Kuna...Huyo ni mwanamke.” Nikaangalia, huyo hapo mwanamume. Nikaiangalia Nuru hiyo, ambayo inaning’inia *hapa*, ikaenda na ikaning’inia juu yake. Nikamwona akijaribu kutoka kitandani, namna hiyo. Jambo ndilo hilo. Mnaona? Huyo hapo. Acha awe ndiye ushahidi. Sivyo? Ulikuwa umeketi, ukiombea hilo. Hiyo ni kweli? Amini kwa moyo wako wote sasa, nawe utapona.

³⁷³ Kwa hiyo, “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.” Iweni tu na imani. Sasa iweni na kicho kabisa.

³⁷⁴ Samahani. Nilikuwa nikiiangalia hiyo Nuru, ikienda huku na huku, kote jengoni. Ni—nilikuwa tu nikiangalia, mnaona.

³⁷⁵ Sasa nataka kuzungumza nawe kwa dakika moja tu. Unaonekana kama ni mtu mzuri, kwangu mimi. Hatufahamiani. [Dada huyo anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Bwana anazijua shida zako. Yeye ananijua mimi, anakujua wewe. Sisi ni mwanamume na mwanamke, tumesimama hapa tumekutana, mara yetu ya kwanza. Kwa Roho, wewe ni Mkristo, na—nami naweza kuhisi mtetemo pale kwa roho yako, wajua, ukisongea tu. Nami ninajua wewe si mwomba lifti. Wewe ni Mkristo, unaona. Kwa hiyo basi hilo ndilo ninalomaanisha, *mwomba*

lifti, ni kuruka kutoka mahali hadi mahali, wajua. Umezaliwa mara ya pili, unaona, wewe ni Mkristo halisi. Ninaweza kuhisi makaribisho yako, unaona. Naye Roho Mtakatifu hapa anaikaribisha roho hiyo, kwa sababu ni roho ya namna moja. Unaona? Sisi ni ndugu na dada. Hupo hapa kwa ajili yako mwenyewe. Umesimama kwa ajili ya mtu mwingine. Rafiki yako anaugua mateso ya pepo. Unaamini hilo? [“Ninajua.”] Wawekee lesu hiyo na usitie shaka, yatawaondokea. Mungu akubariki.

Mwamini Mungu. Amini tu kwa moyo wako wote.

U hali gani, mama? Hatufahamiani mmoja kwa mwingine.

³⁷⁶ Sasa, mtu fulani, mahali fulani. Mungu, yuko wapi? Mahali fulani katika kusanyiko, mtu fulani, jambo fulani lilitukia. “Kwani unajua, Ndugu Branham?” Vema, ninajua tu. Mnaona? Mnaona? Ni kama tu kuuvuta uhai moja kwa moja kutoka kwako, mnaona. Jambo fulani lilitukia. Mtu fulani aliponywa mahali fulani. Sijui ilikuwa ni wapi, lakini labda Yeye atanionyesha tena.

³⁷⁷ Hatufahamiani, mama. Sikujui, bali Mungu anakujua. Uko hapa kwa kusudi fulani, labda kwa ajili ya mtu mwingine, labda matatizo ya kifedha, ya kinyumbani. Yoyote yale, Mungu anaweza kuniambia. Utaamini? Utajua kama ni kweli. Mtu mdogo anazidi kuja hapa, ono linatokea kwa ajili ya mtu mdogo. Sasa, amini kwa moyo wako wote na Mungu atalijalia. Unaona? Kama ninaweza kukwambia, unajua kama sikujui, itabidi itoke kwa nguvu fulani za kimbinguni.

³⁷⁸ Unakumbuka mahubiri yangu usiku wa leo, niliyozungumzia? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Sasa, tazama. Labda, kama ningeweza, kama vile yule Malaika alivyogeuzi mgongo Wake. Sasa, vipi kama nikiugeuzi mgongo wangu, namna *hii*, mahali ulipo. Unaona? Vema. Sasa, wewe mwa—mwambie tu Bwana Yesu, “Ee Mungu,” moyoni mwako tu, “mfunulie Ndugu Branham kile kilichonileta hapa, ama jambo fulani kunihusu mimi,” na uone kama Yeye atanifunulia.

³⁷⁹ Naam. Ninaweza kumwona mwanamke huyo sasa hivi. Yeye anaugua ugonjwa wa matumbo. Hiyo ni kweli. Ni uvimbe katika matumbo. Ni kweli. Bibi Cathan, unaweza kwenda nyumbani sasa na kupata afya, kama utaamini kwa moyo wako wote. Nenda na uamini, uende zako. Liamini.

³⁸⁰ Unaamini? Kuwa na imani. Unatambua ya kwamba yule Mungu hasa aliyeiandika Biblia anatembea katika kanisa hili dogo nyenyekevu hapa usiku wa leo, katika mkutano huu hapa?

³⁸¹ Sasa, hatufahamiani, pia, bwana. Sikujui wewe, sijawahi kukuona maishani mwangu. Hatufahamiani kabisa. Sasa, inanidhoofisha, jamani. Ni. . .

³⁸² Mama huyo anayeketi hapo nyuma amefunga choo, aliyeketi wa pili ndani kutoka kule nyuma, papo hapo kando ya safu ile

pale. Ilikuwa ni wewe, muda mfupi uliopita, uliyekuwa hapa. Kama ukiamini kwa moyo wako wote, kutakuacha.

³⁸³ Vipi kuhusu yule mtoto mchanga mwenye mzio ule? Unaamini Mungu atauponya? Haya basi. Utukufu! Ibilisi alipoteza hilo. Alilipoteza. Mungu akubariki, dada, ndugu. Mwamini Mungu. Hayo tu ndiyo unayohitaji. Utamwacha huyo mtoto. Msisahau.

³⁸⁴ Waligusa nini? Mama huyo aligusa nini, kwa ajili ya mtoto wake mchanga? Siwajui hao watu, kamwe sijawahi kuwaona maishani mwangu.

³⁸⁵ Kama hatufahamiani, inueni mikono yenu hapo, jamani, hapo mahali ilipo. Huyo—huyo mama, inua mkono wako. Hiyo ni kweli.

³⁸⁶ Alikuwa amesimama pale, akimwombea mtoto yule mchanga. Naye Roho Mtakatifu akaendelea kujongea pale, mahali fulani. Ndipo nikaona hapo mahali ilipokuwa, kisha nikamwona huyo mtoto mchanga akiwa—akiwa na hali hiyo. Huyo hapo.

³⁸⁷ Mtoto huyo mchanga atapona, dada. Usifadhaike. Kwa nini? Ni Nuru halisi inayozunguka hapo sasa. Ninajua ya kwamba Mungu alijibu. Mnaona? Utamwacha huyo mtoto mchanga. Ninajua atapata afya. Naam.

³⁸⁸ Inakuja tu kila mahali, kutoka kwenye kusanyiko sasa. Ni, huwezi kuibagua. Iko tu kila mahali. Kuishuhudia tu Hiyo. Hivi hamwamini sasa zaidi ya vile mliyuoamini muda mfupi uliopita? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika. Mnaona Hiyo ni... Linaweza kutukia kwa kila mmoja wenu kama tu mkiamini. Mnaona? Liaminini tu.

³⁸⁹ Kunradhi, bwana. Si—si—sikuninii... Mnajua, sijarukwa na akili. Lakini ninaninii tu... Ninadhoofika kabisa. Nami ninaninii tu...

³⁹⁰ Yesu, mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, Naye akasema, “Naona kwamba nguvu zimenitoka,” hizo ni, uweza. Na ikiwa Yeye, Mwana wa Mungu, vipi kuhusu mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema?

³⁹¹ Sasa, huyu hapa mtu. Jalia litukie kwa mtu huyu. Basi ninyi nyote mtaamini? Kuna mtu anayemfahamu mtu huyu? Yupo mtu anayemfahamu huyu mtu, mahali hapa? Loo, naam, bwana. Vema. Sasa, unajua. Hebu tuone kama ni kweli ama si kweli. Mtu huyu ni mgeni kabisa. Sijawahi kumwona maishani mwangu.

³⁹² Hatufahamiani kabisa. Lakini Roho Mtakatifu anaweza kunifunulia kilichokuleta hapa, ama unachohitaji, ama jambo fulani kukuhusu, ambalo unalijua, ambalo ninajua silijui kabisa, basi hilo lingekushawishi kwamba ingebidi iwe ni Roho Mtakatifu.

393 Lingewashawishi ninyi nyote, na kujua ya kwamba Roho Mtakatifu yeye yule aliye hapa yuko huko nje, pia, ndani yetu sote?

394 Shida yako ni ugonjwa wa rektamu. Ni uvimbe kwenye rektamu. Yupo mtu mwingine hapa anayeliombea hilo, ni mke wako pale nje. Yeye ana maumivu ya kichwa ya kila mara, wakati wote. Hiyo ni kweli. Unaye mtoto mdogo pale, pia. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia mtoto huyo ana shida gani? [Ndugu huyo anasema, “Naam.”—Mh.] Ni ugonjwa wa damu. Unaamini Mungu anaweza kuniambia kuwa wewe ni nani? [“Naam.”] Ungeniamini mimi? Wewe ni mhudumu. [“Naam.”] Wewe ni Kasisi Bw. Mann. [“Naam.”] Nenda nyumbani, ukapate afya.

395 Unaamini kwa moyo wako wote? Mpe tu Mungu sifa.

396 Unaamini, mama, kwa moyo wako wote, unayeketi hapo? Unaamini? Nenda, ukale chakula chako cha jioni. Ugonjwa wako wa tumbo utakuacha, nawe utakuwa mzima.

397 Ugonjwa wako wa mgongo umekuacha pia, dada, kwa hiyo unaweza kupitia tu humu chumbani, na kuamini kwa moyo wako wote kwamba Mungu atakupua afya. Unaamini hilo? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Nenda tu, ukishangilia, na kusema, “Bwana asifiwe!” Vema, kwa moyo wako wote.

398 Wasiwasi ni kitu kibaya, bali Mungu anaweza kuuponya. Unaamini hilo? Nenda tu, ukishangilia, ukisema, “Asante, Bwana.” Mungu anauponya.

399 Maskini tumbo linakusumbua? Nenda, ukale, Yesu Kristo anakuponya. Kuwa na imani.

Mgongo wako unakusumbua. Sivyo? [Mtu huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Nenda, amini. Yesu Kristo anakuponya. Kuwa na imani.

400 Wasiwasi? Unaamini Mungu atakuponya? [Mtu huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Nenda, ukaponywe katika Jina la Yesu.

401 Mnaona ninalomaanisha? Hivi Yesu Kristo si ni yeye yule jana, leo, na hata milele?

402 Sasa, Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Hiyo ni kweli? Sasa, hivi Yesu alisema hivi, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio”? Ni waaminio wangapi waliopo hapa? Vema.

403 Ni wangapi wanaotaka kuponywa? Inueni mikono yenu. Basi wekeaneni mikono. Ninyi ni waaminio. Hiyo ni kweli. Yeye hulitimiza Neno Lake. Mnaamini hilo? Kama mtaliadini, mtaona jambo fulani likitukia ambalo hamjapata kuliona hapo awali, kama mtaamini.

⁴⁰⁴ Sasa inamisheni vichwa vyenu. Wekeni...Usijiombee mwenyewe, mwombee mtu huyo uliyemwekea mikono yako. Ombeni sasa, kwa uaminifu. Aminini, kwa uaminifu. Weka mikono yako juu ya mtu fulani na kuomba. Sasa nitaomba, hapa.

⁴⁰⁵ Baba wa Mbinguni, tunakuja katika Jina la Bwana Yesu. Tunakuja kwa sababu kwamba Neno Lako limethibitishwa. Agizo limethibitishwa. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yuko mbele zetu, katika mfano wa Roho Mtakatifu. Ee Mungu, hawa ni watu Wako. Wanateseka. Shetani amewafunga. Wanajua kwamba Wewe upo hapa. Thibitisho la Uwepo Wako liko hapa, Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.

⁴⁰⁶ Shetani, umeshindwa vita. Toka ndani yao, ewe Shetani, katika Jina la Yesu Kristo. Ninakuapisha uliache kusanyiko hili na utoke ndani ya watu hawa, wapate kuwekwa huru, katika Jina la Yesu Kristo.

⁴⁰⁷ Kama unaamini, simama kwa miguu yako ukampe Mungu sifa. Wazo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo. Inueni mikono yenu na mumpi Yeye sifa. Kuthibitishwa! Kiri na uamini uponyaji wako umekuja. 

62-0122 Kuthibitishwa Kwa Lile Agizo
Assembly Of God
Tempe, Arizona Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org